
Haliuzwi
MEI 13, 2026
/islamicftz
Dhul-Qadah 26 1447
IMAAN
ISSN 5618 - NO. 583
Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

Wapalestina 'wafosi' sala ya Ijumaa Al-Aqsa licha ya vikwazo vya Israel



# Mahujaji 4,000 wa Tanzania tayari kwa safari takatifu

- Waambiwa sio wito wa starehe
- Wausiwa subra, nidhamu, unyenyekevu




Mahujaji 4,500 wa Kenya waifuata Hijja iliyoboreshwa kidijitali

Museveni awapeleka Waislamu 150 Hijja 1447 Makkah

Adabu za safari na hukumu zake

Matukio Yanye Mazigatio »

Nasaha za Wiki »

Visa vya Mitume na Maswahaba »




## Mfumuko wa Bei za Mafuta Wapandisha gharama za gesi

## Dhahabu yainusuru Tanzania kwenye mtikisiko wa soko la mafuta




## Saudi Arabia yakataa anga yake itumike kushambulia Iran


المؤسسة الإسلامية
The Islamic Foundation
KICHINJO CHA MBUZI KWA AJILI YA
Eid Al-Adha
Bei ya MBUZI ni Shilingi
180,000
GHARAMA ZOTE MPAKA KUMFIKIA MLENGWA
MIXX BY YAS
Lipa kwa Simu
Lipa namba:
15441517
Jina la wakala:
The Islamic Foundation
Kwa Mawasiliano Zaidi:
0716 542 323




HABARI
DAR ES SALAAM

NA MWANDISHI WETU

# Mahujaji elfu nne wa Tanzania tayari kwa safari takatifu

- **Waambiwa sio wito wa starehe**
- **Wausiwa subra, nidhamu, unyenyekevu**

Mahujaji zaidi ya 4,000 kutoka Tanzania wameagwa rasmi tayari kuelekea Saudi Arabia kwa ajili ya ibada ya Hijja ya mwaka 1447 Hijria sawa na 2026, huku wakati huohuo taasisi mbalimbali za Hijja zikitumia siku za mwisho kutoa mawaidha, semina na tahadhari kwa mahujaji kabla ya kuanza safari hiyo takatifu.

Hafla kubwa ya kitaifa ya kuwaaga mahujaji hao iliandaliwa na Shirikisho la Taasisi za Hijja Tanzania Bara (TAHAFE) katika Ukumbi wa Mfalme Mohammed VI wa Morocco jijini Dar es Salaam, ambapo mgeni rasmi alikuwa Naibu Qadhi Mkuu wa Tanzania, Sheikh Ally Ngeruko aliyemwakilisha Mufti Mkuu wa Tanzania, Sheikh Abubakar bin Zubeir.

Akizungumza katika hafla hiyo, Sheikh Ngeruko alizitaka taasisi za Hijja kushikamana ili kukabiliana kwa pamoja na changamoto mbalimbali zinazojitokeza wakati wa ibada hiyo. "Umoja wa taasisi utaondosha changamoto za Hijja. Umoja ni nguvu na nguvu kazi yake ni kuzishinda changamoto," alisema na kusisitiza hakuna kikwazo kinaweza kuendelea kuwepo kikikabiliana na nguvu inayotokana na umoja.

Naye Mwenyekiti wa TAHAFE, Haidar Mohammed Kambwili, aliwataka mahujaji kuzingatia nidhamu, kuwatii viongozi wa taasisi zao na kufuata sheria za Saudi Arabia ili kuhakikisha wanatekeleza ibada hiyo kwa utulivu na mafanikio.

"Usigawanye watu kwa misimamo yako... Twaa ni amri. msiwe wababe kwa viongozi," alisema Kambwili huku akisisitiza kuwa viongozi wa taasisi ndio wenye jukumu la kuwaongoza na kuwalinda mahujaji katika mazingira magumu ya Hijja.

Katika tukio jingine, mmoja wa viongozi wa taasisi ya Ahlil Beity Hajj & Umrah, Aisha Idarus, aliwaasa mahujaji kutambua kuwa Hijja si safari ya starehe bali ni ibada inayohitaji uvumilivu, unyenyekevu na kujitoa kwa Allah.

"Hijja si kulala hoteli ya nyota tano wala si safari ya starehe... ni ni taratibu ya ibada, ni safari ya kukutoa katika mazoea yako," alisema Idarus huku akieleza changamoto za mazingira ya Mina na umuhimu wa mahujaji kujitayarisha kiakili na kimwili.

Akifafanua 'kutoka katika mazoea' alisema mwanaume anavuliwa vazi lake, asivae hata nguo ya ndani na badala yake anavaa nguo ya nguo ya ihram, vazi la udhalilifu mkubwa kwa lengo la kumdhalilikia Allah.

Aidha, bi Idarus aliwataka mahujaji kuhakikisha wanakuwa na namba za viongozi wao muda wote pamoja na kutumia teknolojia ya 'location' kwenye simu zao ili kurahisisha msaada endapo watapotea.

Nayo taasisi ya Manasiki Hajj Wal Umrah kupitia semina yake ya kwanza iliyotolewa na Sheikh Awadh Hassan Suru, ilisisitiza umuhimu wa subra katika utekelezaji wa ibada hiyo.

Sheikh Suru alisema mafanikio ya Hijja yanategemea uwezo wa mahujaji kuvumilia mazingira magumu, ucheleweshaji wa huduma na changamoto mbalimbali bila kuingia katika migogoro. Alinukuu aya ya 197 ya Suratul Baqarah inayokataza maneno machafu, vitendo viovu na mabishano wakati wa Hijja.

"Mambo matatu haya yanahitaji subira," alisema huku akiwataka mahujaji kujiepusha na hasira, ubishi na kufanya maamuzi binafsi bila ushauri wa viongozi wao.

Ukiacha subira, Sheikh huyo aliwahimiza mahujaji kuwatii viongozi na kuwa na upendo, huruma na unyenyekevu miongoni mwao na kwa mahujaji wenzao kutoka nchi mbalimbali watakaokutana nao huko Makka.

Sheikh Suru aliwasisitizia mahujaji wakumbuke malengo ya Hijja. "Sisi hapa wote lengo letu kutekeleza nguzo hii ya nne ni kutaka kufutiwa madhambi ili turejee kama siku tulipozaliwa na mama zetu. Hakuna kitu kingine tunakitafuta. Nani sasa yuko tayari kujipamba na subra, utii, na unyeneyevu, ili kupata msamaha wa Allah Mtukufu na kurejea yuko mweupe? Kila mmoja ajipange katika hilo," alihoji na kuhamasisha.

Katika semina nyingine iliyoandaliwa na iTravel Hajj and Umrah, mwanazuoni Sheikh Twaha Suleiman Bane aliwahimiza mahujaji kusikiliza kwa makini mafunzo ya Hijja ili waweze kutekeleza ibada hata wakitenganishwa na makundi yao.

Sheikh Bane pia alisisitiza umuhimu wa adabu na heshima katika ibada hiyo, akiwataka mahujaji kuepuka kuwaudhi wengine wakati wa kutekeleza ibada mbalimbali ikiwemo kubusu Hajar al-Aswad.

Kipekee, alielezea umuhimu wa siku ya Arafa akisema ni siku ya msamaha mkubwa mbele ya Allah na akawahimiza mahujaji kuitumia kwa dua, toba na ibada badala ya kupoteza muda katika mazungumzo yasiyo na faida.

Naye Alhaj Sheikh Hassan Katungunya wa Zamzam Centre Hajj and Umrah aliwasihi mahujaji kumuomba Allah awarejeshe tena katika ardhi takatifu siku zijazo kwa ajili ya Hijja na Umrah. "Sema, 'Ya Rabbi nirejeshe tena nipe sababu za kurudi katika ibada hii, nipe sababu za kurudi katika miji hii," alisema huku akieleza kuwa dua ya ikhlas inaweza kuwa sababu ya Muislamu kupata fursa nyingine ya kurejea Makka na Madina.

Huko Zanzibar, Qadhi Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Hassan Othman Ngwali, akiwaaga mahujaji kupitia Kidundo Hajj & Umrah Travel Agency, alisisitiza umuhimu wa nidhamu na kuwatii viongozi.

"Tusiwe vikwazo kwa kutowasikiliza viongozi," alisema Sheikh Ngwali huku akiwataka mahujaji kujadiliana na viongozi wao kabla ya kufanya maamuzi binafsi.

Aliongeza: "Ukiamriwa aidha fuata ulichoambiwa au fikra yako mpe kiongozi akukinaishe au umkinaishe, baada ya hapo mtakayokubaliana ndio lifanyike. Isiwe unafata fikra yako ilhali ushapewa maelekezo mengineLikikufika, linakuwa lako peke yako," alisema.

Kadhalika, aliwataka mahujaji kuepuka kuwaudhi wengine katika utekelezaji wa ibada, akitoa mfano, ni bora kukosa sunna ya kubusu Hajar al-Aswad kuliko kufanya kitendo cha haramu cha kuwasukuma au kuwaumiza watu wengine.

ذو القعدة

HABARI
DAR ES SALAAM

NA MWANDISHI WETU



# Elimu yatajwa kuamsha hamasa Hijja Tanzania ikiifukuzia Kenya

Naibu Qadhi Mkuu wa Tanzania, Sheikh Ally Ngeruko amesema kampeni za utoaji elimu kuhusu Hijja zimechangia ongezeko kubwa la idadi ya Watanzania wanaokwenda kutekeleza ibada hiyo takatifu katika miaka ya karibuni.

Sheikh Ngeruko alisema kupitia programu ya "Elimu Kwanza" iliyokuwa ikitumika kutoa elimu, hamasa na uelewa kuhusu Hijja, idadi ya mahujaji imeongezeka kutoka wastani wa watu 3,000 hadi zaidi ya 4,000 wanaotarajiwa kwenda mwaka huu.

Alitoa kauli hiyo katika hafla ya kuwaaga mahujaji takriban 4,000 wanaotarajiwa kuelekea Saudi Arabia kwa ajili ya Hijja ya mwaka huu, hafla iliyoandaliwa na Shirikisho la Hijja Tanzania Bara (TAHAFE) katika Ukumbi wa Msikiti wa Mfalme Mohammad VI, Kinondoni jijini Dar es Salaam.

"Tukielimisha zaidi, watu wataamka usingizini watakuja kujiunga kwenda kumuabudu Mwenyezi Mungu," alisema Sheikh Ngeruko huku akizitaka taasisi zinazoshughulikia Hijja kuongeza juhudi katika utoaji wa elimu kwa umma.

Aidha, aliitaka TAHAFE kuandaa bajeti maalum kwa ajili ya kusambaza elimu ya Hijja kuelekea misimu ijayo, huku akipendekeza wanachama wote 18 wa shirikisho hilo wachangie mfuko huo.

Sheikh Ngeruko alisema Tanzania ina vijana wengi wa Kiislamu wenye uwezo mkubwa wa kushawishi jamii lakini bado hawajatumika ipasavyo katika kazi ya utoaji elimu na hamasa kuhusu Hijja.

Alisisitiza umuhimu wa kutumia vyombo vya habari na teknolojia za mawasiliano katika kueneza elimu hiyo, ikiwemo televisheni, redio, machapisho, tovuti, mitandao ya kijamii pamoja na mihadhara ya ana kwa ana.

"Mmejitambua mkabadilika. Mkaanza kutoa elimu, matunda mmeyaona. Badilikeni sasa. Acheni tu kukalia viti. Pangeni programu za mambo mbalimbali – kutoa elimu, kushawishi watu, kutengeneza raha zaidi," alisema.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na viongozi wa dini, waumini pamoja na ndugu wa mahujaji waliokusanyika kuwaombea safari njema na mafanikio katika ibada hiyo ya Hijja.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa TAHAFE, Haidar Mohammed Kambwili alisema idadi ya mahujaji kutoka Tanzania Bara imeongezeka kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na miaka ya nyuma ambapo waliokuwa wakisafiri walikuwa kati ya watu 600 hadi 700 pekee.

Hata hivyo, Kambwili alikiri kuwepo kwa changamoto za kiutendaji katika usimamizi wa Hijja kati ya Tanzania Bara na Zanzibar, ingawa alisema hatua zinaendelea kuchukuliwa kuzitatua.

Licha ya mafanikio hayo, Tanzania bado iko nyuma ya Kenya kwa idadi ya mahujaji inaowapeleka Saudi Arabia kila mwaka.

Kwa mujibu wa taarifa za Kenya Hajj Mission chini ya SUPKEM, Kenya mwaka huu inatarajia kupeleka mahujaji takriban 4,500 kwa ajili ya Hijja ya 2026, ikiwa ni zaidi ya idadi ya Tanzania inayokadiriwa kufikia zaidi kidogo ya mahujaji 4,000.

Kenya ina Waislamu asilimia takriban 11 kati ya wananachi wote wanaokadiriwa kufikia Milioni 59, ilhali takriban nusu ya Watanzania wote wanaokadiriwa kufikia Milioni 73 ni Waislamu.

Kwa upande wa Uganda, nchi hiyo mwaka huu inatarajia kupeleka mahujaji 1,546 baada ya Mamlaka ya Uganda Bureau of Hajj Affairs (UBHA) kuthibitisha kuwa mahujaji wote wamekamilisha taratibu za visa na vibali vya safari. Viongozi wa Kiislamu nchini humo pia wameonya kuhusu mawakala wasio rasmi wa Hijja huku wakisifu maboresho ya usimamizi wa safari hizo yaliyosaidia kuondoa changamoto zilizokuwa zikijitokeza miaka ya nyuma.

Uganda yenyewe inatajwa kuwa na Waislamu asilimia 14 kati ya wananchi wake wapatao Milioni 53.

ذو القعدة

KUTOKA KWA MAJIRANI

NA MUGINI SINGIRA

# Mahujaji 4,500 wa Kenya waifuata Hijja iliyoboreshwa kidijitali

Waislamu 4,500 kutoka Kenya wanatarajiwa kushiriki ibada ya Hijja mwaka 2026 huku mamlaka za Saudi Arabia zikianza matumizi makubwa ya mfumo wa kidijitali wa NUSUK unaolenga kuimarisha usalama, uratibu na ustawi wa mahujaji wakati wa ibada hiyo kubwa zaidi ya kidini duniani.

Kundi la kwanza la mahujaji kutoka Kenya linatarajiwa kuondoka Mei 7 kuelekea Saudi Arabia, kuanza safari ya kiroho inayowakusanya mamilioni ya Waislamu katika mji mtakatifu wa Makkah kwa ajili ya kutekeleza ibada ya Hijja, moja ya nguzo tano za Uislamu.

Mwenyekiti wa Kenya Hajj Mission ambaye pia ni kiongozi wa Baraza Kuu la Waislamu Kenya (SUPKEM), Hassan Ole Naado, alisema Kenya imefanikiwa kutumia nafasi zote 4,500 zilizotengwa kwa mwaka huu.

"Hija ni moja ya ibada muhimu zaidi katika Uislamu, na tunafurahia kuwa Kenya imefanikiwa kutumia kikamilifu nafasi zake mwaka huu," alisema Ole Naado.

Alisema mahujaji wote wanapitia mafunzo maalumu yanayosimamiwa na mawakala wa Hijja yaliyoandaliwa kuwajengea uelewa kuhusu ibada za Hijja pamoja na masuala ya vitendo kama safari, malazi, usimamizi wa misongamano na mazingira ya Saudi Arabia.

Ole Naado aliwataka mahujaji kudumisha nidhamu, subira, heshima na mshikamano wakati wote wa ibada hiyo, akisisitiza kuwa Hijja inahitaji uvumilivu wa kimwili pamoja na maadili mema.

Mwaka huu, mahujaji wa Kenya watanufaika na maboresho mbalimbali yaliyofanywa na Wizara ya Hijja na Umra ya Saudi Arabia chini ya mpango wa Vision 2030, ukiwemo mfumo wa NUSUK ulioboreshwa kutoka programu ya Eatmarna mwaka 2022.

Mfumo huo unatumia kadi maalumu za kidijitali zenye QR Code zinazorahisisha utambuzi wa mahujaji, huduma za usafiri, malazi na usimamizi wa safari kati ya maeneo matakatifu ya Mina, Arafat na Muzdalifah. Aidha, mfumo huo unasaidia kupunguza msongamano kwa kupanga ratiba maalumu za matembezi ya mahujaji, huku mamlaka za Saudi Arabia zikitumia kamera za kisasa zenye teknolojia ya akili bandia (AI) kufuatilia mkusanyiko wa watu katika maeneo ya ibada kwa wakati halisi.

Saudi Arabia pia imeboresha miundombinu katika maeneo matakatifu kwa kuweka mifumo ya kisasa ya kupunguza joto, ikiwemo miamvuli mikubwa na vifaa vya kutoa hewa yenye ukungu katika Msikiti wa Namira uliopo Arafat ili kusaidia mahujaji kukabiliana na joto kali wakati wa ibada.

# Museveni awapeleka Waislamu 150 Hijja Makkah



Rais wa Uganda, Yoweri Kaguta Museveni, amedhamini Waislamu 150 kwenda kutekeleza ibada ya Hijja katika mji mtakatifu wa Makkah, Saudi Arabia, mwaka huu katika mpango uliolenga kusaidia Waumini wasiokuwa na uwezo kumudu gharama za safari hiyo takatifu.

Kundi la kwanza la mahujaji 90 liliondoka rasmi Mei 6 baada ya kuagwa mjini Kampala na Mshauri Mkuu wa Rais anayeshughulikia uhamasishaji wa kisiasa, Moses Byaruhanga, huku kundi la pili likitarajiwa kuondoka Mei 12.

Byaruhanga alisema gharama zote za Hijja hiyo zimelipwa na Rais Museveni na kwamba safari ya Hijja kwa mtu mmoja hugharimu wastani wa shilingi milioni 21 za Uganda, sawa na zaidi ya shilingi bilioni tatu kwa mahujaji wote 150.

"Badala ya nafasi 100 za kawaida, mwaka huu Rais amefadhili Waislamu 150 kwenda Hijja," alisema Byaruhanga.

Aliongeza kuwa Serikali imeendelea kushirikiana na Baraza Kuu la Waislamu Uganda (UMSC) kuhakikisha uchaguzi wa wanufaika unafanyika kwa uwazi kupitia viongozi wa Kiislamu wa kila eneo.

Aidha, alisema Serikali imeendelea kuunga mkono maendeleo ya Waislamu kupitia mfumo wa benki za Kiislamu na mikopo isiyo na riba kwa SACCO za viongozi wa Kiislamu.

Msaidizi Maalumu wa Rais anayehusika na habari na uhamasishaji, Haji Faruk Kirunda, aliwataka mahujaji kufuata sheria za Saudi Arabia na kuepuka tabia zinazoweza kuharibu taswira ya Uganda. "Msijione watalii. Mkikiuka sheria tunaweza kurudi bila nyinyi baada ya Hijja," alisema. Baadhi ya wanufaika walieleza furaha yao kwa kupata nafasi hiyo. Mayimuna Nababi kutoka Mukono alisema hakutarajia kupata fursa hiyo.

"Namshukuru Rais Museveni kwa zawadi hii. Allah amenijaalia kutimiza ndoto yangu," alisema.

Kwa upande wake, Sheikh Kassim Kigozi kutoka Butambala alisema alipitwa na nafasi hiyo mwaka jana lakini sasa amefanikiwa kwenda Hijja kupitia ufadhili huo wa Serikali.

**HABARI**
**DAR ES SALAAM**

NA MWANDISHI WETU

# Dhahabu yainusuru Tanzania kwenye mtikisiko wa soko la mafuta

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imesema ongezeko la mauzo ya dhahabu linaendelea kulilinda taifa dhidi ya mshtuko wa bei ya mafuta duniani unaosababishwa na mvutano wa kisiasa Mashariki ya Kati na usumbufu wa usafirishaji kupitia Mlango wa Hormuz.

Ripoti ya BoT ya Aprili 2026 inaonyesha kuwa dhahabu imekuwa chanzo kikuu cha utulivu wa uchumi wa nje, ikichangia asilimia 30 hadi 40 ya mapato ya fedha za kigeni ya Tanzania. Mapato ya dhahabu yamepanda kutoka dola bilioni 3.77 (2025) hadi dola bilioni 5.2 (2026).

Mgogoro wa Mlango wa Hormuz, unaopitisha takriban asilimia 20 ya mafuta duniani, umeongeza bei ya mafuta, mbolea na gharama za usafirishaji duniani, hali inayoongeza mfumuko wa bei na gharama za maisha.

BoT inasema ongezeko la bei ya mafuta linaathiri karibu sekta zote za uchumi kutokana na gharama za usafirishaji, huku kaya za kipato cha chini zikitarajiwa kuathirika zaidi.

Hata hivyo, mapato ya dhahabu yameongeza akiba ya fedha za kigeni na kusaidia kupunguza shinikizo la uagizaji mafuta na bidhaa nyingine muhimu.

Gavana wa BoT Emmanuel Tutuba amesema bila mchango wa dhahabu, gharama za kuagiza bidhaa muhimu zingekuwa kubwa zaidi, akisisitiza haja ya kuimarisha upatikanaji wa fedha za kigeni na mfumo wa benki ili kudumisha uthabiti wa uchumi.

■ **Gavana wa BoT Emmanuel Tutuba amesema bila mchango wa dhahabu, gharama za kuagiza bidhaa muhimu zingekuwa kubwa zaidi, akisisitiza haja ya kuimarisha upatikanaji wa fedha za kigeni na mfumo wa benki ili kudumisha uthabiti wa uchumi.**



NA MWANDISHI WETU

# Mfumuko wa Bei za Mafuta Wapandisha Gharama za gesi

Kupanda kwa bei za mafuta duniani kumeanza kuathiri sekta mbalimbali za uchumi, huku athari za hivi karibuni zikionekana kwenye ongezeko la bei ya gesi ya kupikia (LPG), nishati safi ambayo serikali imekuwa ikiihamasisha kwa nguvu chini ya ajenda yake ya nishati safi ya kupikia.

Ongezeko hilo linaongeza mzigo kwa kaya nyingi ambazo tayari zinakabiliwa na gharama kubwa za maisha, na kulazimisha baadhi ya familia kutafakari upya matumizi yao ya nishati za kila siku.

Wakala wa gesi kutoka maeneo mbalimbali nchini wamethibitisha kupanda kwa bei hizo, ingawa kampuni kadhaa za LPG zimekanusha kutangaza rasmi ongezeko hilo.

Meneja wa Masoko wa Oryx Energies, Bw. Peter Ndomba, alisema kampuni hiyo haijatoa taarifa yoyote rasmi kuhusu mabadiliko ya bei.

Kwa upande wake, ofisa wa TotalEnergies ambaye hakutaka kutajwa jina alisema kampuni hiyo haijapandisha bei, huku jitihada za kuwapata maofisa wa Puma Energy zikigonga mwamba.

Hivi karibuni, Taifa Gas iliwahakikishia watumiaji kuwa itaendelea kudumisha bei nafuu licha ya kupanda kwa gharama kwenye soko la dunia.

Kwa mujibu wa muundo mpya wa bei, mtungi wa kilo sita umeongezeka kutoka Sh24,000 hadi Sh28,000, huku wa kilo 15 ukipanda kutoka Sh58,000 hadi Sh63,000. Mtungi wa kilo 38 sasa unauzwa hadi Sh145,000 kwa watumiaji wa mwisho.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Bw. Gerald Maganga, alisema mamlaka hiyo inaendelea kufuatilia mwenendo wa bei za LPG katika soko la dunia na kulinganisha na bei za ndani ili kulinda maslahi ya watumiaji.

Wataalamu wa uchumi wameonya kuwa ongezeko hilo linaweza kuongeza gharama za uzalishaji na huduma, hali itakayoweza kuchochea mfumuko wa bei.

**Kwa mujibu wa muundo mpya wa bei, mtungi wa kilo sita umeongezeka kutoka Sh24,000 hadi Sh28,000, huku wa kilo 15 ukipanda kutoka Sh58,000 hadi Sh63,000. Mtungi wa kilo 38 sasa unauzwa hadi Sh145,000 kwa watumiaji wa mwisho.**



NA MWANDISHI WETU

# Zanzibar mwenyeji wa mkutano wa forodha duniani

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kwa mara ya kwanza imeandaa mkutano wa Shirika la Forodha Duniani Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika (WCO ESA).

Mkutano huo ulianza Mei 7, 2026 na unatarajiwa kumalizika Mei 15, 2026 visiwani Zanzibar, ukishirikisha wajumbe zaidi ya 100.

Kamishna wa Forodha na Ushuru wa Bidhaa, Juma Bakari, amesema mbali na manufaa ya kiforodha, mkutano huo pia una manufaa ya kiuchumi kwa Tanzania kupitia sekta mbalimbali, ikiwamo utalii.

Amesema kupitia mkutano huo, nchi wanachama 24 zinazounda umoja wa ESA zitawasilisha taarifa za utekelezaji wa maazimio yaliyofikiwa katika kikao kilichopita na kujadili utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Uongozi la 31 yaliyotolewa Mei 2025 nchini Afrika Kusini.

Kwa upande wake, kiongozi wa Shule ya Ushuru nchini Kenya ambaye ni miongoni mwa watoa mada, Dkt. Emma Omwenga, amesema mafunzo hayo yanatolewa ili kuhakikisha mipaka inalindwa sambamba na afya za wananchi wa mataifa husika.

Mkutano wa WCO ESA umetanguliwa na mkutano wa wakufunzi wa vituo vya mafunzo ya forodha vya kanda na utafuatiwa na mkutano wa 43 wa wataalamu wa masuala ya forodha na kuhitimishwa na Mkutano wa 32 wa Baraza la Uongozi.



NA YUSUPH AMIN

# Serikali yaja na mkakati mpya wa afya kupitia vipaumbele 11



**VIPAUMBELE VINAENDANA NA:**

- Dira ya Taifa 2050
- Mpango wa Nne wa Taifa wa Maendeleo
- Ilani ya CCM ya 2025–2030
- Ajenda ya Rais Samia Suluhu Hassan

Tanzania inaendelea kuimarisha ufadhili wa maendeleo katika sekta ya afya huku ikielekea kupanua bima ya afya kwa wote, kuongeza uzalishaji wa dawa ndani ya nchi na kuimarisha huduma za tiba bingwa na ubingwa bobezi.

Waziri wa Afya, Mohamed Mchengerwa, jana aliwasilisha bungeni bajeti ya Sh trilioni 1.8 kwa mwaka wa fedha 2026/27, akieleza vipaumbele 11 vya kimkakati vinavyolenga kubadili utoaji wa huduma za afya na kuiweka Tanzania kuwa kitovu cha huduma za tiba katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Kati ya fedha hizo, Sh trilioni 1.15 zimetengwa kwa matumizi ya maendeleo, ikiwa ni ongezeko kidogo kutoka Sh trilioni 1.14 zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2025/26.

Bw. Mchengerwa alisema vipaumbele hivyo vinaendana na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Mpango wa Nne wa Taifa wa Maendeleo, Ilani ya CCM ya 2025–2030 pamoja na ajenda ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuimarisha huduma za jamii na maendeleo ya rasilimali watu.

Moja ya maeneo makuu ya kipaumbele ni utekelezaji wa mpango wa Bima ya Afya kwa Wote (UHI), ambao serikali imesema utaongeza upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi wote bila kujali uwezo wa kipato.

"Serikali itaendelea kutekeleza mpango wa Bima ya Afya kwa Wote kwa kusajili wananchi kutoka kaya zenye uhitaji na zile zenye uwezo, huku ikiimarisha mifumo endelevu ya kugharamia huduma za afya," alisema.

Alisema hadi sasa serikali imetumia Sh bilioni 48.8 katika mpango huo, ambapo kaya 172,297 zimeshafikiwa na walengwa 463,228 wameweza kupata huduma katika vituo vya afya vilivyosajiliwa.

Katika kupunguza utegemezi wa dawa kutoka nje ya nchi, serikali imepanga kuwekeza katika uzalishaji wa dawa ndani ya nchi, ikiwemo ujenzi wa maabara ya kisasa ya utafiti wa dawa na kuongeza uwezo wa uzalishaji wa dawa za ARV katika kiwanda cha Tanzania Pharmaceutical Industries.

Mkakati huo pia utahusisha majukwaa ya uwekezaji kwa ajili ya kuvutia wawekezaji wa ndani na nje katika sekta ya dawa, pamoja na kuboresha mifumo ya ununuzi na usambazaji wa dawa.

Kipaumbele kingine kikubwa ni upanuzi wa huduma za tiba bingwa na ubingwa bobezi ili kupunguza rufaa za wagonjwa kwenda nje ya nchi na kukuza utalii wa matibabu.

Serikali imepanga kuongeza huduma katika hospitali za rufaa za mikoa, kanda na taifa, huku vituo maalumu vya ubora vikianzishwa kwa ajili ya matibabu ya magonjwa ya moyo, upandikizaji figo, upandikizaji uboho na huduma za afya ya kinywa na meno.

Idadi ya hospitali za rufaa za mikoa zinazotoa huduma za tiba bingwa itaongezeka kutoka nane hadi 17, huku hospitali tano za wilaya zikianza kutoa huduma maalumu za kibingwa.

Upanuzi huo utaungwa mkono na uwekezaji katika vifaa vya kisasa vya uchunguzi, mifumo ya maabara, huduma salama za damu na uwezo wa uhandisi wa vifaa tiba.

Katika eneo la rasilimali watu, wizara imepanga kuongeza mafunzo ya udaktari bingwa pamoja na kuajiri watumishi zaidi wa afya kwa ajira za kudumu na mikataba.

Bajeti hiyo pia imeweka mkazo katika afya ya mama na mtoto kupitia upatikanaji bora wa vifaa vya afya ya uzazi, upanuzi wa vitengo vya watoto wachanga na kuimarisha huduma za wakunga kwa lengo la kupunguza vifo vya mama na mtoto mchanga.

Katika kudhibiti magonjwa, serikali itaongeza ufuatiliaji na mifumo ya mwitikio wa haraka kwa magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza, huku ikiajiri wahudumu 8,000 wa afya ngazi ya jamii.

Mifumo ya afya kidijitali nayo itapanuliwa, ikiwemo mfumo wa kielektroniki wa ufuatiliaji wa chanjo, huduma za tiba kwa njia ya mtandao (telemedicine) na kanzidata ya taifa ya afya itakayosaidiwa na teknolojia ya akili bandia (AI).

Huduma za afya ya akili pia zimepewa nafasi, ambapo serikali imepanga kuandaa mkakati wa taifa wa afya ya akili na msaada wa kisaikolojia pamoja na kuboresha huduma za urekebishaji kwa makundi yenye uhitaji maalumu.

Kwa mujibu wa bajeti hiyo, Sh bilioni 652.2 zitatumika kwa matumizi ya kawaida huku Sh trilioni 1.148 zikielekezwa kwenye miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo, Sh bilioni 789.4 zitatoka ndani ya nchi na Sh bilioni 358.5 kutoka kwa wahisani na mikopo ya nje. Wizara pia inatarajia kukusanya mapato ya Sh bilioni 747.2 katika mwaka huo wa fedha.

SEHEMU YA
2

Na Said Rajab
0783 650 803

# Faida 10 za ibada ya Hijja

**Katika sehemu ya kwanza ya makala haya wiki iliyopita, tuliangazia baadhi ya faida kubwa zitokanazo na ibada ya Hijja, zikiwamo kusamehewa madhambi, kuingia Peponi na kujibiwa dua. Katika sehemu hii ya pili na ya mwisho, tutataja faida nyingine za ibada hiyo muhimu.**



# Faida 10 za ibada ya Hijja




## Mwenendo sahihi

Ibada ya Hijja hutupatia fursa ya kufurahia maisha yenye uwiano mzuri, huku ikitusaidia kupata mafanikio duniani kwa kuendeleza haiba njema, kwani Hijja hutufunza mwenendo mwema.

Allah 'Azza Wajallah' ametuamrisha kushikamana na tabia njema kama masurufu bora katika safari ya Hijja.

Anasema: "Hijja ni miezi maalumu. Na anayekusudia kufanya Hijja katika miezi hiyo, basi asiseme maneno machafu wala asifanye vitendo vichafu wala asibishane katika Hijja. Na kheri yoyote mnayofanya Mwenyezi Mungu anaijua. Na chukueni masurufu (ya kutumia njiani). Na hakika bora ya masurufu ni uchamungu. Na nicheni Mimi, enyi wenye akili." [Qur'an, 2:197].

Waislamu wanaotekeleza Hijja wanatakiwa kuzingatia nidhamu, subira, wema, uvumilivu na zaidi ya yote amani. Wanapaswa kudumisha amani kwao wenyewe, kwa wanyama na viumbe hai wengine, wakiwamo wadudu. Hii ina maana kwamba wanapaswa kudhibiti hasira zao.

Kudhibiti hasira ni tabia ambayo Waislamu wanapaswa kuikuza hata katika miezi mingine ya mwaka. Kutoka kwa Abu Huraira (Allah amridhie) amesema, mtu mmoja alikwenda kwa Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) akamuomba amuusie jambo lolote. Mtume alimwambia: "Usikasirike." Yule mtu akarudia tena ombi lake, Mtume akamwambia kwa mara nyingine: "Usikasirike." [Bukhari].

Katika hadith nyingine, Mtume amesema: "Mwenye nguvu si yule anayewashinda watu kwa nguvu zake, bali ni yule anayeweza kujidhibiti anapokuwa na hasira." [Bukhari na Muslim].

## Kuongeza imani

Kutekeleza ibada ya Hijja huongeza imani na kutufanya tutambue namna Allah anavyowatendea kwa haki waja wote wanaomuabudu na kuwafanya kuwa sawa.

Waislamu kutoka pande zote za dunia, bila kujali rangi, kabila, taifa au hadhi ya kijamii na kiuchumi, huvaa mavazi yanayofanana, husoma dua zilezile, hutamka takbira ileile na kutekeleza vipengele vilevile vya ibada ya Hijja kwa lengo moja la kumridhisha Muumba.

Waislamu wanaokwenda Hijja hushuhudia mkusanyiko mkubwa wa watu kutoka mataifa mbalimbali ambao hakuna dini nyingine duniani iliyowahi kuushuhudia.

Tunaposhuhudia watu kutoka nchi tofauti wakitekeleza ibada ya Hijja kwa ajili ya kumridhisha Mwenyezi Mungu, tunapata ushahidi kwamba Uislamu ni dini ya ulimwengu mzima.

Hijja hutupatia fursa ya kusafiri na kukutana na ndugu zetu Waislamu kutoka mataifa mbalimbali, jambo linalotuwezesha kujuana, kusaidiana na kuboresha mitazamo yetu ya kijamii na kiutamaduni.

Hali hiyo inaonesha mshikamano wa kindugu uliopo miongoni mwa Waislamu. Allah anasema: "Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanaume na mwanamke. Na tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika mbora wenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule aliye mchamungu zaidi kati yenu..." [Qur'an, 49:13].

"..na saidianeni katika wema na uchamungu. Wala msisaidiane katika dhambi na uadui. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu." [Qur'an, 5:2].

## Mazoezi ya ukakamavu

Hijja hutufunza ukakamavu, jambo ambalo Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) amelihimiza aliposema: "Muumini mwenye nguvu ni bora na anapendwa zaidi na Allah kuliko muumini dhaifu..." [Sahih Muslim].

Kuizunguka Ka'aba mara saba, kutembea kati ya Safa na Marwa, kusafiri kutoka Msikiti Mkuu wa Makka kwenda Mina, Arafa na Muzdallifah, kurusha vijiwe pamoja na kuswali sala za kila siku, yote hayo hutupatia fursa ya kuwa wakakamavu.

Ni lazima tuwe na nguvu na kujiandaa kupambana na shetani, washirika wake na wale wanaofuata nyayo zake.

Allah 'Azza Wajallah' anatukumbusha kuhusu uovu wa shetani: "Na ambao hutoa mali yao kwa kuonesha watu, wala hawamuamini Mwenyezi Mungu wala Siku ya Mwisho, na yule ambaye shetani amekuwa ndiye rafiki yake, basi ana rafiki mbaya mno." [Qur'an, 4:38].

Mwenyezi Mungu ametubainishia kuwa shetani ni adui yetu wa wazi: "Hakika shetani ni adui yenu, basi mfanyeni kuwa adui. Kwani yeye analiita kundi lake liwe katika watu wa Motoni." [Qur'an, 35:6].

Shetani huamrisha mambo maovu na machafu, hivyo tunapaswa kuwa na nguvu ili tuweze kumuabudu Allah 'Azza Wajallah' kwa kadri ya uwezo wetu na hatimaye kupata Pepo yake. Tunapaswa pia kuwa na nguvu katika kuamrisha mema na kukemea maovu ili tuwe miongoni mwa waja bora mbele ya Allah.

*Itaendelea katika toleo lijalo, Insha Allah.*

## HUDUMA ZA KIFEDHA ZA KIISLAMU

UKHTI FATIMA SS




# Standard Chartered yatuzwa Benki Bora ya Kiislamu, Sukuk Yenye Ubunifu

Benki ya Standard Chartered imetajwa kuwa "Benki Bora ya Kiislamu ya Mwaka" huku ikitwaa pia tuzo ya "Sukuk Yenye Ubunifu Zaidi" kutoka jarida la kimataifa la The Banker kutokana na mafanikio yake katika huduma za fedha za Kiislamu duniani.

Tuzo hizo zimetolewa kwa kutambua uwezo wa benki hiyo kutoa huduma zinazozingatia sheria za Kiislamu katika maeneo mbalimbali ya Asia, Afrika na Mashariki ya Kati.

Standard Chartered imeendelea kuimarisha nafasi yake katika sekta ya fedha za Kiislamu kwa kuhudumia wateja binafsi wenye uwezo mkubwa kifedha pamoja na taasisi na kampuni kubwa zinazohitaji mitaji kupitia mifumo inayokubaliana na Sharia.



Mtendaji Mkuu wa Kitengo cha Benki ya Kiislamu wa Standard Chartered, Khurram Hilal, alisema sekta ya fedha za Kiislamu inaendelea kubadilika na kuwa mfumo wa kimataifa unaovuka mipaka ya nchi moja moja.

"Wateja binafsi wanawekeza zaidi katika masoko ya kimataifa huku taasisi zikihitaji vyanzo mbalimbali vya mitaji na ukwasi," alisema Hilal.

Alisema nguvu ya benki hiyo ipo katika uwezo wake wa kuunganisha malengo ya biashara na uzingatiaji madhubuti wa misingi ya Sharia kupitia jukwaa moja la huduma za kifedha.

Tuzo hizo zinakuja wakati sekta ya fedha za Kiislamu ikiendelea kuwa miongoni mwa sekta zinazokua kwa kasi duniani, huku thamani ya mali zake ikitarajiwa kuongezeka kwa asilimia 36 na kufikia dola trilioni 7.5 ifikapo mwaka 2028.

## Indonesia yataka kuimarisha huduma za afya zinazozingatia Sharia

**Serikali ya Indonesia imesisitiza umuhimu wa kuimarisha huduma za afya zinazozingatia misingi ya Sharia ili kukidhi mahitaji ya kimatibabu pamoja na mahitaji ya kiroho ya wananchi wake.**

**Naibu Waziri wa Afya wa Indonesia, Dante Saksono Harbuwono, alisema huduma za afya nchini humo zinapaswa kutoa utulivu, heshima na huduma zinazoendana na maadili ya wagonjwa.**

**Alisema kwa kuwa asilimia 87 ya wananchi wa Indonesia ni Waislamu, nchi hiyo ina nafasi kubwa ya kuwa kitovu cha kimataifa cha utalii wa afya wa halal.**

**Harbuwono alisema hospitali zinazozingatia Sharia hazipaswi kuangalia tiba na teknolojia pekee bali pia huduma za kibinadamu na ustawi wa kiroho wa wagonjwa.**

**Alibainisha kuwa hospitali 24 nchini humo tayari zimepata vyeti vya huduma za afya zinazozingatia Sharia katika maeneo mbalimbali ya Java, Sumatra na Kalimantan.**

**Aidha, alisema Indonesia inalenga kuhakikisha bidhaa takribani 44,000 za dawa zinapata vyeti vya halal ifikapo mwaka 2026 huku Serikali ikiendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuimarisha mfumo wa afya wa halal nchini humo.**

## Nigeria yalenga soko la nyama ya halal la dola trilioni 2

**Nigeria imeanza mikakati ya kujipatia sehemu ya soko la kimataifa la nyama ya halal linalokadiriwa kuwa na thamani ya zaidi ya dola trilioni mbili kwa kuimarisha sekta ya mifugo, mifumo ya uthibitishaji na uwekezaji katika uzalishaji wa nyama inayokidhi viwango vya Kiislamu. Hatua hiyo inakuja wakati mahitaji ya bidhaa za halal yakiongezeka duniani kutokana na kuongezeka kwa idadi ya Waislamu pamoja na ongezeko la watumiaji wanaotaka bidhaa salama na zenye viwango vya ubora.**

**Mkuu wa Operesheni wa Dar Al Halal Certification, Dk. Maiyaki Sani, alisema Nigeria ina nafasi nzuri ya kijiografia kusambaza nyama ya halal katika masoko makubwa kama Saudi Arabia, UAE, Qatar, Malaysia na Indonesia.**

**Alisema ushindani katika soko la halal sasa unategemea zaidi uaminifu wa uthibitishaji, ubora wa bidhaa na uwezo wa kufuatilia mnyororo mzima wa uzalishaji. Kwa mujibu wa wachambuzi, Nigeria pia inanufaika na idadi kubwa ya mifugo inayozidi milioni 200 huku matumizi ya nyama yakifikia tani milioni 1.5 kwa mwaka.**

## Ivory Coast kupanua mfumo wa benki kujumuisha fedha za Kiislamu

**Makumi ya maelfu ya Waislamu Ijumaa walikusanyika katika Msikiti wa Al-Aqsa uliopo Jerusalem kwa ajili ya swala ya Ijumaa licha ya vikwazo vikali vya usalama vilivyowekwa na vikosi vya Israel. Kwa mujibu wa shirika la habari la Palestina, WAFA, waumini hao walianza kuwasili mapema asubuhi katika eneo la msikiti huo huku wakikabiliwa na ukaguzi mkali wa kijeshi na vizuizi katika malango ya kuingia ndani ya Al-Aqsa.**

**Taarifa hiyo ilisema vikosi vya Israel viliongeza uwepo wa wanajeshi ndani na pembezoni mwa Mji wa Kale wa Jerusalem katika kile kinachotajwa kuwa hatua ya kuimarisha usalama.**

**Licha ya masharti hayo, maelfu ya waumini waliendelea kufika kwa ajili ya kutekeleza ibada ya swala ya Ijumaa katika eneo hilo takatifu ambalo ni miongoni mwa maeneo muhimu zaidi**

NA UKHTI FATIMA



**Kwa muda mrefu, baadhi ya viongozi wa taasisi na kampuni wamekuwa wakiamini kuwa ukali, presha na usimamizi wa kibabe ndiyo siri ya kupata matokeo mazuri kazini. Lakini tafiti nyingi za kisasa sasa zinaonyesha kuwa mazingira ya kazi yenye heshima, kujali na utu huongeza zaidi tija, ubunifu na ufanisi wa wafanyakazi kuliko mazingira ya hofu. Wafanyakazi wanapohisi kuthaminiwa, kusikilizwa na kuheshimiwa, huwa na motisha kubwa zaidi ya kufanya kazi kwa moyo. Lakini wanapofanya kazi katika mazingira ya dharau, vitisho au kulaumiwa kila wakati, nguvu nyingi za akili hutumika kupambana na msongo wa mawazo badala ya ubunifu na uzalishaji.**

**Ndiyo maana wataalamu wa saikolojia ya kazi wanaeleza kuwa "kindness in the workplace" yaani utamaduni wa wema kazini si jambo la anasa, bali ni sehemu muhimu ya mafanikio ya taasisi.**

# Kujali, kutendea wema wafanyakazi huongeza tija, ufanisi

Moja ya mambo muhimu katika kujenga mazingira mazuri ya kazi ni kuhakikisha wafanyakazi wanapata taarifa muhimu kwa wakati. Katika sehemu nyingi za kazi, matatizo huanza pale watu wanapohisi wameachwa gizani kuhusu maamuzi yanayowahusu. Kukosa taarifa huzaa hofu, uvumi na kutokuaminiana.

Lakini kiongozi anayewashirikisha wafanyakazi wake katika taarifa na mawasiliano hujenga hisia ya umiliki na ushirikiano. Mfanyakazi anapojua kuwa sauti yake ina thamani, huwa tayari zaidi kushiriki katika mafanikio ya taasisi.

Pia, sehemu ya kazi yenye afya huwa ni ile inayotoa nafasi kwa kila mtu kuchangia mawazo yake. Wakati mwingine viongozi husikiliza watu wale wale kila siku huku wengine wakinyamaza kwa hofu au kuona mawazo yao hayana maana. Lakini ukweli ni kwamba hata mfanyakazi wa chini kabisa anaweza kuwa na wazo linaloweza kuleta mabadiliko makubwa.

Kuwasikiliza watu ni aina ya heshima. Na watu wanapoheshimiwa, huongeza kiwango cha kujituma.

Katika mazingira mengi ya kazi, watu huzoea kuona makosa haraka kuliko juhudi nzuri. Mfanyakazi anaweza kufanya kazi nzuri kwa miezi mingi bila kuambiwa neno lolote, lakini akifanya kosa dogo tu hukosolewa hadharani. Hali hiyo huondoa hamasa na kuua morali taratibu.

Lakini viongozi wenye hekima hutambua nguvu ya pongezi. Kumwambia mfanyakazi, "Asante kwa kazi nzuri," au "Umejitahidi sana hapa," kunaweza kuongeza ari ya kazi kwa kiwango kikubwa kuliko watu wengi wanavyodhani. Binadamu wana hitaji la ndani la kuthaminiwa.

Hii haimaanishi kufumbia macho makosa. Hapana. Kazi bado inahitaji uwajibikaji na viwango. Lakini hata kurekebisha makosa kunaweza kufanywa kwa utu na heshima bila kumdhalilisha mtu.

Pia, sehemu ya kazi yenye mafanikio si ile isiyo na migogoro, bali ni ile inayojua namna ya kushughulikia migogoro kwa utulivu. Watu wanapokoseana, badala ya kushambuliana au kutafuta wa kulaumiwa, viongozi bora hujenga mazungumzo ya kutafuta suluhisho.

Kuuliza, "Tunaweza kujifunza nini hapa?" mara nyingi hujenga maendeleo kuliko kuuliza, "Nani mwenye kosa?"

Wema kazini pia huonekana pale viongozi na wafanyakazi wanapojaribu kuelewa hali za wenzao. Mfanyakazi anaweza kuonekana mwenye hasira, mchovu au mwenye makosa mengi si kwa sababu ni mzembe, bali kwa sababu anapitia changamoto nzito binafsi. Huruma kidogo inaweza kubadilisha kabisa namna mtu anavyofanya kazi.

Katika mtazamo wa Kiislamu, kuwatendea watu kwa ihsani na maneno mazuri ni sehemu ya maadili mema. Mtume Muhammad (rehema na amani zimshukie) alikuwa mwenye upole kwa watu wake, mwenye kusikiliza na mwenye kuwathamini waliofanya kazi pamoja naye. Hata alipokosoa, alifanya hivyo kwa hekima na heshima.

Katika dunia ya sasa yenye ushindani mkubwa wa kiuchumi, taasisi nyingi zinawekeza kwenye teknolojia na mifumo ya kisasa lakini zinasahau jambo moja muhimu: wafanyakazi ni binadamu kabla ya kuwa mashine za uzalishaji.

Na mara nyingi, mfanyakazi anayejisikia kuthaminiwa huongeza tija kuliko anayefanya kazi kwa hofu.

MAHMOUD NYAMGUMA



# Saudi Arabia yakataa anga yake itumike kushambulia Iran

Saudi Arabia imekanusha taarifa zinazoeleza kuwa imefungua anga yake kwa ajili ya operesheni za kijeshi za mashambulizi huku mvutano ukiendelea kati ya Marekani na Iran katika eneo la Strait of Hormuz.

Chanzo kisichotajwa jina kilichonukuliwa na televisheni ya Al-Hadath kilisema Saudi Arabia haijaruhusu matumizi ya anga yake kusaidia mashambulizi ya kijeshi na kwamba msimamo wa Riyadh unabaki kuwa kuunga mkono juhudi za kupunguza mvutano na mazungumzo ya amani.

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Saudi Arabia anayehusika na diplomasia ya umma, Rayed Krimly, pia alisisitiza kupitia mtandao wa X kuwa Saudi Arabia inaendelea kuhimiza mazungumzo, utulivu na kuepuka kuongezeka kwa mzozo.

Kauli hizo zimekuja baada ya gazeti la Wall Street Journal kuripoti kuwa Saudi Arabia na Kuwait zimeondoa vikwazo vya matumizi ya kambi za kijeshi na anga kwa ndege za Marekani kufuatia operesheni inayojulikana kama “Project Freedom”.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, maafisa wa Pentagon wanatazamia kuanza tena operesheni hiyo katika siku za karibu.

Hata hivyo, Saudi Arabia imeendelea kusisitiza kuwa inaunga mkono suluhisho la kidiplomasia katika mgogoro wa Marekani na Iran na inapinga mashambulizi dhidi ya miundombinu ya kiraia katika eneo hilo.

# Pakistan yaonya mienendo ya uvamizi wa kijeshi Israel

Pakistan imelionya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuwa upanuzi wa makazi haramu ya Israel katika Ukingo wa Magharibi unazidi kuharibu matumaini ya kuundwa kwa dola huru ya Palestina.

Balozi wa Pakistan Umoja wa Mataifa, Asim Iftikhar Ahmad, amesema Israel inabadili uvamizi wa muda kuwa umiliki rasmi kupitia sheria mpya, uporaji wa ardhi na kuwafukuza Wapalestina katika maeneo yao ya kihistoria.

Kwa mujibu wa takwimu za Umoja wa Mataifa, mashambulizi ya walowezi wa Kiyahudi dhidi ya Wapalestina mwaka 2025 yalifikia kiwango cha juu zaidi tangu mwaka 2006.

Pakistan imesema ndani ya miaka minne, Israel imeidhinisha makazi mapya 102 katika ardhi za Palestina, jambo linalokiuka Mkataba wa Nne wa Geneva na sheria za kimataifa.

Mradi tata wa makazi wa E-1 karibu na Mashariki mwa Jerusalem umetajwa kuwa tishio kubwa kwa uwezekano wa kuwepo taifa lenye muunganiko wa kijiografia kwa Wapalestina.

Akizungumza katika kikao kilichoandaliwa na mataifa kadhaa ya Ulaya, Pakistan imesisitiza kuwa suluhisho la kudumu ni kuondoka kwa Israel katika maeneo iliyoyakalia tangu mwaka 1967 na kuanzishwa kwa taifa huru la Palestina lenye mji mkuu wake Mashariki mwa Jerusalem.

# Misri yachukizwa
## Iran kushambulia UAE

Misri imelaani vikali mashambulizi ya Iran dhidi ya Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) yaliyosababisha majeruhi huku ikisisitiza mshikamano wake kamili na taifa hilo la Ghuba.

Katika taarifa iliyotolewa Ijumaa kupitia shirika la habari la MENA, Serikali ya Misri ilisema mashambulizi hayo ni ukiukwaji wa wazi wa mamlaka na uhuru wa UAE pamoja na kuvunja sheria za kimataifa na Mkataba wa Umoja wa Mataifa.

Misri ilieleza kuwa mashambulizi hayo yanatishia usalama na utulivu wa eneo la Mashariki ya Kati na yanaweza kudhoofisha juhudi za kikanda na kimataifa zinazolenga kupunguza mvutano.

Taarifa hiyo iliongeza kuwa kuendelea kwa mashambulizi hayo ni hatua ya hatari inayoweza kuongeza hali ya sintofahamu katika eneo hilo ambalo tayari linakabiliwa na migogoro ya kisiasa na kijeshi.

ذو القعدة



MAHMOUD NYAMGUMA

# Wapalestina 'wafosi' sala ya Ijumaa Al-Aqsa licha ya vikwazo vya Israel



Makumi ya maelfu ya Waislamu Ijumaa walikusanyika katika Msikiti wa Al-Aqsa uliopo Jerusalem kwa ajili ya swala ya Ijumaa licha ya vikwazo vikali vya usalama vilivyowekwa na vikosi vya Israel.

Kwa mujibu wa shirika la habari la Palestina, WAFA, Waumini hao walianza kuwasili mapema asubuhi katika eneo la msikiti huo huku wakikabiliwa na ukaguzi mkali wa kijeshi na vizuizi katika malango ya kuingia ndani ya Al-Aqsa.

Taarifa hiyo ilisema vikosi vya Israel viliongeza uwepo wa wanajeshi ndani na pembezoni mwa Mji wa Kale wa Jerusalem katika kile kinachotajwa kuwa hatua ya kuimarisha usalama. Licha ya masharti hayo, maelfu ya Waumini waliendelea kufika kwa ajili ya kutekeleza ibada ya swala ya Ijumaa katika eneo hilo takatifu ambalo ni miongoni mwa maeneo muhimu zaidi kwa Waislamu duniani.

Msikiti wa Al-Aqsa umekuwa ukishuhudia mvutano wa mara kwa mara kati ya Wapalestina na mamlaka za Israel, hasa wakati wa ibada kubwa za Kiislamu.

## Saudi Arabia yaisaidia Syria sekta ya elimu

**Shirika la Misaada la Saudi Arabia, KSrelief litakarabati shule pamoja na vituo vya kijamii katika majimbo ya Idlib na Deir ez-Zor nchini Syria, hatua itakayoimarisha matumaini ya maelfu ya wananchi waliodhoofishwa na vita vya muda mrefu.**

**Miradi hiyo inatarajiwa kuwafikia moja kwa moja zaidi ya watu 4,990 huku karibu wananchi 19,894 wakinufaika kwa njia zisizo za moja kwa moja.**

**Taarifa mbalimbali zinasema zaidi ya watoto milioni 2.4 nchini Syria bado wanakosa elimu ya kawaida kutokana na uharibifu wa shule na athari za vita vilivyochukua zaidi ya muongo mmoja.**

**Katika mazingira hayo, Saudi Arabia imeendelea kujijengea taswira ya mshirika muhimu wa Waislamu wa Syria kwa kuwekeza katika ujenzi wa shule 48, madarasa ya muda, pamoja na mifumo ya nishati ya Jua inayolenga kuimarisha mazingira ya kujifunzia kwa watoto waliopoteza matumaini.**

**Mbali na elimu, KSrelief pia imeongeza juhudi katika sekta ya afya na huduma za dharura. Mwezi uliopita, taasisi hiyo ilizindua mpango wa kitabibu wa kujitolea unaohusisha miradi 53 katika taaluma 239 za afya na ufundi, huku zaidi ya wananchi 18,000 wakitarajiwa kunufaika.**

ذو القعدة

## KUTOKA KWA MHARIRI

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
+255 789 201383

# Kila la heri mahujaji; msisahau kuiombea dunia amani

Msimu wa Hijja umewadia, na tayari baadhi ya Waislamu wapo katika ardhi tukufu ya Makka kwa ajili ya kutekeleza ibada ya Hijja. Kwa hakika, ni safari ya siku chache lakini yenye tija na umuhimu mkubwa mno.

Pamoja na Hijja kuwa fursa ya kuijua historia ya tauhidi, yaani kumpwekesha Mwenyezi Mungu, ibada hiyo pia huwakumbusha mahujaji wajibu wao wa kuishi chini ya ngao ya umoja, ambao ni msaada mkubwa katika kulinda undugu na mshikamano miongoni mwa Waislamu.

Si hivyo tu, bali Hijja huwafunza namna ya kujizatiti vilivyo katika majukumu ya Uislamu na kujitoa muhanga. Ni kwa msingi huo, Allah Ta'ala amewaamuru Waislamu wote wenye uwezo wa kwenda Hijja kufanya hivyo.

Sisi, gazeti la Imaan, tunawatakia kila la heri mahujaji wote kutoka Tanzania Bara na Visiwani, pamoja na ulimwengu mzima katika safari hii tukufu ya kuitikia wito wa Muumba wetu wa kwenda kuizuru Nyumba yake Tukufu (Al-Kaaba).

Pamoja na kuwepo kwa changamoto zinazojitokeza kila mwaka kabla na wakati wa Hijja, mahujaji wanapaswa kujitahidi kufuata kanuni, adabu na miiko ya ibada hiyo kama ilivyothibiti kwa Mtume (Allah amshushie rehema na amani).

Kama inavyojulikana, hekima kubwa ya Hijja ni kumfanya mja kudhihirisha utumishi wake kwa Mwenyezi Mungu, jambo linaloshuhudiwa katika siku zote za ibada hiyo.

Kwa minajili hiyo, tunawakumbusha mahujaji kwamba katika kipindi chote watakachokuwa katika miji Mitakatifu ya Makka na Madina, watumie vyema fursa hiyo kwa kujikurubisha zaidi kwa Allah Ta'ala kwa kufanya kheri mbalimbali.

Pia tunamuusia kila hujaji asitafute kuitwa Al-Hajj au Hajjat, bali ajitahidi kurekebisha mwenendo wake na kudumisha yale aliyojifunza katika ibada hiyo katika maisha yake yote.

Kwa kuzingatia hali ya migogoro na vita vinavyoshuhudiwa katika maeneo mbalimbali duniani, kuna umuhimu kwa mahujaji kuyaombea mataifa amani katika ibada zao, kwani Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Mahujaji na wenye kufanya Umra ni wageni wa Allah. Wanachomuomba anawapa, na wakimtaka msamaha anawasamehe." [An-Nasai, Ibn Majah, na wengineo].

Mwisho, tunamuomba Allah awape mahujaji wote unafuu na wepesi katika safari yao na katika utekelezaji wa jukumu hilo tukufu, na awasamehe madhambi yao.

Vilevile, tunamuomba awakubalie Hijja yao, na baada ya kukamilika kwa ibada hiyo awajaalie kurejea katika miji yao wakiwa na ufahamu mpana kuhusu nguzo ya Hijja na Uislamu kwa ujumla. Aidha, tunamuomba Allah Ta'ala awawezeshe Waislamu ambao hawakubahatika kutekeleza Hijja mwaka huu kufanya hivyo kabla ya kuondoka duniani.



2149953422

SHEIKH Shaaban Mussa
0786 272 323

# Istiqamah, kusimama imara baada ya Ramadhan

Miongoni mwa alama kubwa ya mafanikio ya Ramadhan si tu kufanya ibada kwa wingi ndani ya mwezi huo mtukufu, bali ni uwezo wa Muislamu kuendelea kusimama imara katika njia ya Mwenyezi Mungu hata baada ya Ramadhan kuisha.

Hii ndio inaitwa istiqamah — yaani, kuwa na msimamo thabiti katika dini ya Allah bila kuyumba au kurudi nyuma. Wapo walioitaja kama uadilifu wa ndani unaoonekana katika matendo ya nje.

Tukifafanua zaidi, istiqamah ni hali ya mtu kuendelea kuwa mnyoofu katika utiifu kwa Mwenyezi Mungu, akizingatia amri Zake na kujiepusha na makatazo Yake katika kila hali ya maisha; iwe yuko nyumbani, kazini, au hata akiwa peke yake pasipo kuonekana na watu wengine.

Ndani ya Ramadhan, Muislamu hujijenga katika misingi ya kheri kwa nidhamu ya hali ya juu: huswali kwa wakati, husoma Qur'an kwa wingi, hujizuia na maasi, na huongeza ibada za sunna kwa juhudi kubwa.



Hata hivyo, kipimo cha kweli cha mafanikio ya Ramadhan si yale aliyoyafanya ndani ya mwezi huo pekee, bali ni mwenendo wake baada ya Ramadhan kuisha.

Changamoto kubwa si kuanza njia ya haki, bali ni kuendelea nayo kwa uthabiti bila kuchoka au kukata tamaa. Wengi huanza kwa ari na nguvu ndani ya Ramadhan, lakini baada ya mwezi huo kuisha, huanza kulegea taratibu hadi baadhi yao hurudi katika hali yao ya zamani. Huu ni udhaifu wa msimamo na kukosekana kwa istiqamah.

Mwenyezi Mungu Ameamrisha waja Wake kuwa na msimamo thabiti pale aliposema: "Basi simameni imara kama mlivyoamrishwa." Hii ni ishara wazi kuwa Uislamu si dini ya msimu maalum kama Ramadhan pekee, bali ni mfumo wa maisha ya kila siku, mwaka mzima.

Ili kufikia istiqamah, ni lazima kuwa na nia thabiti na juhudi endelevu, nalo si jambo rahisi, kwani linahitaji mapambano dhidi ya nafsi na vishawishi vya dunia.

Muislamu anatakiwa kujiwekea malengo ya kufanya wema mdogo lakini wa kudumu, kwani wema wa kudumu una thamani kubwa zaidi kuliko ule mkubwa unaokatika.

Moja ya sababu zinazowafanya watu kukosa istiqamah ni kurudi katika mazingira mabaya baada ya Ramadhan. Marafiki wasiofaa, vikao visivyo na manufaa, pamoja na matumizi mabaya ya muda vinaweza kumrudisha mtu nyuma na kuvunja yale aliyoyajenga kwa bidii ndani ya mwezi mtukufu.

Hivyo basi, ili kudumisha msimamo, ni muhimu kuchagua mazingira bora na kuzungukwa na watu wema wanaokukumbusha kumcha Mwenyezi Mungu. Rafiki mwema ni hazina kubwa katika safari ya imani, kwani humsaidia mtu kubaki katika njia ya haki hata anapodhoofika.

Aidha, kujikumbusha malengo ya Akhera mara kwa mara kunasaidia sana kudumisha istiqamah. Muislamu akitambua kuwa maisha ya dunia ni ya muda mfupi na kwamba kuna siku ya hisabu mbele ya Mwenyezi Mungu, atakuwa makini zaidi katika matendo yake na ataepuka kurudia makosa.

Pia, ni muhimu kuendelea na ibada ndogo ndogo lakini za kudumu, kama vile kuswali sunna, kusoma Qur'an hata aya chache kila siku, kufanya dhikri, na kutoa sadaka inapowezekana. Ibada hizi hujenga msingi imara wa imani na humsaidia mtu kubaki katika mstari sahihi kwa muda mrefu.

Istiqamah pia inahusisha kutokata tamaa pale mtu anapoteleza. Binadamu si mkamilifu, na makosa ni sehemu ya maisha. Lakini tofauti anayoonesha Muumini, anapotenda kosa, hurejea haraka kwa Mwenyezi Mungu kwa toba ya dhati na kuendelea mbele bila kukata tamaa.

Kwa hakika, msimamo thabiti ndio unaoonesha ubora wa imani ya mtu. Si lazima kuanza kwa nguvu kubwa sana, bali muhimu zaidi ni kudumu katika njia ya haki hadi mwisho.

Hivyo basi, baada ya Ramadhan, kila Muislamu anapaswa kujiuliza kwa dhati: Je, bado ninasimama imara katika ibada zangu? Je, yale niliyojifunza katika Ramadhan bado nayatekeleza? Au tayari nimeanza kuyumba taratibu bila kutambua?

Ni kwa kujitathmini mara kwa mara ndipo mtu anaweza kurekebisha mwenendo wake na kurejea katika mstari sahihi. Istiqamah si jambo la siku moja, bali ni safari ya maisha inayohitaji subira, juhudi, na kumtegemea Mwenyezi Mungu kila wakati.

Lakini pamoja na msimamo katika ibada binafsi, kuna somo jingine kubwa ambalo Ramadhan hujenga ndani ya jamii nzima ya Waislamu — nalo ni umoja na mshikamano.

Katika makala inayofuata, tutazungumzia kuhusu Umoja wa Kiislamu – Matunda ya Ramadhan katika jamii, na jinsi ya kuudumisha baada ya mwezi mtukufu kuisha.

# ذوالقعدة فتاوى



**SHEIKH**
**Shaaban Mussa**
**0786 272 323**

## Swali: Ni ipi hukumu ya kula viumbe wa baharini kama samaki, chaza (kombe), kaa wa bahari, kamba (lobster) na pweza? Je, ni kweli pweza ni haramu?

**Jibu:** Kwa mujibu wa dalili za Qur'an na Sunna, asili ya vyakula vya baharini ni halali.Mwenyezi Mungu amesema: "Mmehalalishiwa kuvua baharini na kula vilivyomo humo kama starehe kwenu na kwa wasafiri." [Qur'an, 5: 96].

Na Mtume (rehema amshushie rehema na amani) amesema: "Maji yake ni safi ya kujitwaharisha, na maiti wake ni halali." [Abu Daud na wengine].

Kauli ya wanazuoni, na hukumu ya pweza

Jamhuri ya wanazuoni (Malik, Shafi'i na Hanbali) wanaona kuwa kila kinachoishi baharini pekee ni halali kuliwa, iwe ni samaki, chaza, kaa, kamba (lobster), pweza na wengineo—mradi hakina madhara kwa afya.

Hata hivyo, madhehebu ya Hanafi na baadhi ya wanazuoni wa Kishia wanaweka mipaka zaidi, wakihalalisha hasa samaki, na kutokubaliana kuhusu baadhi ya viumbe wengine wa baharini.

Kwa mujibu wa Jamhuri ya wanazuoni, pweza ni halali kwa kuwa ni miongoni mwa viumbe wa baharini. Hakuna dalili inayotenga pweza na viumbe wengine wa baharini waliohalalishwa, isipokuwa kama itathibitika kuwa na madhara au sumu.

Ama kuhusu aya zinazotaja "nyama laini ya baharini", zimekuja kuelezea neema ya Mwenyezi Mungu, si kuweka sharti la uhalali. Hivyo, si lazima kila kiumbe wa baharini awe na "nyama laini" ili aruhusiwe kuliwa.

Kuhitimisha, niseme kuwa kwanza, asili ya vyakula vya baharini ni halali; hivyo, samaki, chaza, kaa, kamba (lobster) na pweza ni halali kwa mujibu wa Jamhuri ya wanazuoni. Kila chenye madhara au sumu hakiruhusiwi.Tofauti katika jambo hili ni za kielimu kati ya madhehebu, na si katazo la jumla.

Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

## Swali: Kuna mtu ninaymdai kiasi kikubwa cha fedha, na anatarajia kulipa, lakini kwa sasa hana uwezo wa kulipa. Wakati huo huo, huyu mdaiwa anastahiki kupokea zaka, je, ninaweza kumfutia sehemu ya deni ninalomdai na nikalihesabu kuwa hiyo ndiyo zaka yangu kwake? Au nimpe zaka kutoka mali nyingine tofauti na deni hilo?

Jibu: Kinachofaa kwako ni kumpa zaka kutoka mali uliyonayo, ikiwa yeye ni miongoni mwa wanaostahiki zaka. Ama kufuta deni alilonalo kisha ukalihesabu kuwa ni zaka, hilo halitoshelezi (halikubaliki kama zaka) kwa sababu zaka ni kutoa na kumpa mtu mali, siyo kusamehe deni.

Deni alilonalo linafaa apewe muda ikiwa hana uwezo wa kulipa, mpaka atakapoweza. Mwenyezi Mungu anasema: "Na ikiwa (mdaiwa) ana shida, basi apewe muda mpaka apate nafuu." [Qur'an, 2:280]. Kuhusu zaka, hakuna ubaya kumpa kutoka katika zaka ikiwa anastahiki (kwa mfano akiwa maskini), lakini si sahihi kufuta deni kisha ukalihesabu kuwa ni zaka. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

## Swali: Je, deni linatolewa zaka au halitolewi?

Jibu: Deni lina ufafanuzi wa aina tofauti. Ikiwa deni liko kwa mtu asiye na uwezo wa kulipa (maskini), au kwa watu wanaochelewesha kulipa bila haki, basi halitolewi zaka mpaka mwenye deni aipokee haki yake. Akishaipokea, ndipo aanze kuhesabu mwaka mpya wa kutoa zaka.

Lakini ikiwa deni liko kwa mtu mwenye uwezo wa kulipa na akidaiwa hulipa, basi deni hilo linatolewa zaka. Yaani inahesabika kama vile mali iliyo kwenye amana kwa mtu fulani, hivyo mtu atatoa zaka yake pindi mwaka unapokamilika.

Ama deni lililo kwa asiye na uwezo wa kulipa halitolewi zaka, kwa sababu mali hiyo iko hatarini, haijulikani kama itapatikana au la. Vivyo hivyo kwa mtu mwenye uwezo lakini anachelewesha kulipa, huyu pia hukumu yake ni kama asiye na uwezo. Allah tunamuomba atuepushe na hayo.

## Swali: Ni ipi hukumu ya deni ambalo limekaa mwaka mzima likiwa kwa mdaiwa, nami sijalipokea? Je, nitoe zaka au nifanyeje?

**Jibu:** Ikiwa deni liko kwa mtu asiye na uwezo wa kulipa, basi halina zaka mpaka upokee. Vivyo hivyo ikiwa deni liko kwa mtu anayekataa au kuchelewesha kulipa, huna wajibu wa kutoa zaka mpaka ulipwe, kisha uanze kuhesabu mwaka mpya.

Lakini ikiwa deni liko kwa mtu mwenye uwezo na hacheleweshi kulipa —yaani ukimdai anakulipa— basi ni lazima utoe zaka pindi mwaka unapokamilika, hata kama hujalipokea, kwa sababu ni kama mali iliyopo mikononi mwako. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

ذُو القِعْدَة

NASAHA
ZA WIKI
0787 503 085



NA YUSUFU AMINI

# Teknolojia ya WiFi: Uwiano kati ya fursa na hatari kwa vijana

Katika ulimwengu wa sasa kunaoshuhudia maendeleo makubwa ya teknolojia, matumizi ya mtandao wa WiFi yamekuwa sehemu ya maisha ya kila siku kwa watu wa rika zote. Vijana na watoto ndiyo wanaotumia zaidi teknolojia hii, wakivutiwa na urahisi wa kupata taarifa, burudani na mawasiliano kupitia simu janja, kompyuta na vifaa vingine vya kidijitali.

Kwa mujibu wa tathmini ya kitafiti iliyofanywa mwaka 2024, watoto wenye umri wa miaka 8 hadi 10 hutumia hadi saa nane kwenye mitandao ya kijamii, jambo ambalo si jema.

Hata hivyo, pamoja na faida nyingi za WiFi, kumekuwa na ongezeko la matumizi hasi yanayosababisha athari mbaya katika makuzi ya vijana na ustawi wa watoto.

Kwanza, matumizi mabaya ya WiFi yanahusishwa kwa karibu na uraibu wa mtandao. Watoto na vijana wengi hutumia muda mwingi mitandaoni wakifuatilia mitandao ya kijamii, kucheza michezo ya video au kutazama video bila kikomo.

Tabia hii hupunguza muda wa kushiriki shughuli muhimu kama kusoma, kucheza michezo ya nje, na kuwasiliana ana kwa ana na familia na marafiki. Uraibu huu unaweza kuathiri uwezo wa mtoto kujifunza na kuzingatia masomo darasani.

Aidha, WiFi imekuwa lango la kufikia maudhui yasiyofaa kwa watoto. Kupitia mtandao, watoto wanaweza kufikia picha, video au maandishi yenye maudhui ya vurugu, ngono au lugha chafu.

Maudhui haya yanaweza kuathiri maadili ya mtoto na kumfanya aige tabia zisizofaa. Katika baadhi ya matukio, watoto huanza kuonesha mienendo ya ukatili au kukosa heshima kwa wakubwa kutokana na kile wanachokiona mtandaoni.

Pia, kuna hatari ya unyanyasaji wa mtandaoni (cyberbullying) ambao umeenea kutokana na matumizi ya WiFi. Vijana wanaweza kutumiwa ujumbe wa kejeli, vitisho au fedheha kupitia mitandao ya kijamii na majukwaa ya mawasiliano.

Athari zake ni pamoja na msongo wa mawazo, kutojiamini na hata mawazo ya kujiua kwa baadhi ya waathirika. Kwa watoto, hali hii huwa ngumu zaidi kwa kuwa hawana uwezo wa kujilinda kikamilifu.

Matumizi ya WiFi pia yamechangia kupungua kwa shughuli za kimwili. Badala ya watoto kucheza nje, kukimbia au kushiriki michezo mbalimbali, wengi wao hukaa ndani wakitumia vifaa vyao kwa muda mrefu.

Hali hii husababisha matatizo ya kiafya kama unene uliopitiliza, matatizo ya macho, na usingizi usio wa kawaida. Madaktari wamekuwa wakionya kuhusu athari za muda mrefu za matumizi ya kupita kiasi ya skrini kwa watoto.

Kwa upande mwingine, kuna changamoto ya usalama wa taarifa binafsi. Watoto na vijana mara nyingi hawana uelewa wa kutosha kuhusu namna ya kulinda taarifa zao mtandaoni, hali inayowafanya kuwa rahisi kulengwa na matapeli au wahalifu wa mtandaoni.

Zaidi ya hayo, matumizi mabaya ya WiFi yanaweza kuathiri uhusiano wa kifamilia. Wazazi wengi wanalalamika kuwa watoto hutumia muda mwingi kwenye simu au kompyuta badala ya kushiriki mazungumzo ya kifamilia.

Hali hii hupunguza ukaribu na mawasiliano ndani ya familia, na inaweza kusababisha kutokuelewana au migogoro ya mara kwa mara. Familia inapopoteza muda wa pamoja, malezi bora ya watoto huathirika.

Kwa upande wa elimu, wanafunzi hutumia intaneti kudurufu kazi za shule bila kuelewa, jambo linalodhoofisha uwezo wao wa kufikiri na ubunifu. Aidha, baadhi yao hutumia muda wa masomo kuperuzi mitandao ya kijamii, hali inayoshusha kiwango cha ufaulu darasani.

Licha ya changamoto hizi, ni muhimu kutambua kuwa WiFi si adui; tatizo kubwa liko katika matumizi yake yasiyo sahihi. Wazazi, walimu na jamii kwa ujumla wana jukumu la kuwaongoza watoto na vijana kutumia teknolojia kwa njia salama na yenye manufaa.

Elimu kuhusu matumizi sahihi ya mtandao inapaswa kuanza mapema, huku wazazi wakifuatilia na kudhibiti muda ambao watoto wanatumia mtandaoni.

Isitoshe, Mwenyezi Mungu Mtukufu ameonya kuhusu kulinda macho na nyoyo zetu kwa kusema: “(Ewe Nabii) waambie waumini wanaume wainamishe macho yao na wahifadhi tupu zao...” [Qur’an, 24:30].

“Na waambie waumini wanawake wainamishe macho yao na wahifadhi tupu zao, na wala wasidhihirishe mapambo yao...” [Qur’an, 24:31]. Aya hizi zinaonesha umuhimu wa kuepuka kuangalia mambo maovu ambayo mara nyingi hupatikana kirahisi kupitia mitandao.

Aghlabu, watoto na vijana hupoteza muda mwingi kwenye intaneti na hivyo kupuuza majukumu yao ya ibada na masomo. Mwenyezi Mungu anasema katika sura ya Al–Isra [Qur’an, 17:36]: “Na wala usifuate yale usiyo na ujuzi nayo...”, akisisitiza matumizi bora ya muda na akili katika mambo yenye manufaa.

Na katika hadith iliyonukuliwa na Tirmidhi, Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: “Miongoni mwa uzuri wa Uislamu wa mtu ni kuacha yasiyomhusu.” Kwa hiyo, ni muhimu kwa wazazi na walezi kuweka mipaka na kufuatilia matumizi ya WiFi ili kuhakikisha watoto wanaitumia kwa mambo yenye manufaa.

Aidha, serikali ina wajibu wa kuweka sera na mifumo madhubuti ya kulinda watoto dhidi ya maudhui hatarishi, ikiwemo kuweka vikwazo vya maudhui, kuhimiza matumizi ya programu za udhibiti wa wazazi (parental controls) na kuendesha kampeni za uhamasishaji kuhusu usalama mtandaoni.

ذوالقعدة

MAKALA MAALUM



SHEIKH
Seif Ruga
0712 690 811

# Adabu za safari na hukumu zake

**Allah Mtukufu amewaamuru waja wake kusafiri katika ardhi kwa madhumuni ya kuchunguza na kuzingatia neema zake pamoja na ustadi wa uumbaji wake. Anasema Allah: "...tembeeni katika ardhi na tazameni jinsi (Allah) alivyoanzisha uumbaji." [Qur'an, 29:20]. Vilevile, Allah anasema: "Yeye ndiye aliyeidhalilisha ardhi kwa faida yenu, basi tembeeni katika pande zake, na kuleni katika riziki zake. Na kwake Yeye mtafufuliwa." [Qur'an, 67:15].**

Safari humpa mwanadamu fursa ya kujitenga na shughuli za kila siku na changamoto za maisha. Imam Shafi (Allah amrehemu) amesema: "Safari ina faida tano; kuondoa huzuni, kupata riziki, kupata elimu, kujifunza adabu, na kupata marafiki wema."

Aidha, safari ni njia ya kutafakari maajabu ya dunia na kujenga imani thabiti kwa Allah Mtukufu, ikithibitisha kwamba dunia hii ina Mfalme na Mtawala Mkuu anayestahili kuabudiwa peke yake. Allah anasema: "Na katika ardhi kuna ishara (mazingatio) kwa wenye kuamini." [Qur'an, 51:20].

Kwa Muislamu, sababu za kusafiri ni nyingi, miongoni mwazo ni kutekeleza ibada ya Hijja au Umra, kutafuta elimu au riziki, pamoja na kutembelea ndugu, jamaa na marafiki.

## Adabu za safari

### Mosi, nia njema

Mtume wa Allah (rehema na amani zimshukie) amesema: "Vitendo vinategemea (vinalipwa kwa) nia, na kila mtu atapata kwa mujibu wa alichokusudia." [Bukhari na Muslim]. Kwa mantiki hiyo, msafiri anapaswa kuzingatia kwa makini madhumuni ya safari yake yawe halali; na ikiwa ni safari ya mapumziko, ni lazima azingatie mipaka ya sharia na kuepuka vitendo vya ufujaji.

### Pili, maandalizi

Ni sunna kwa msafiri kujiandaa vyema na safari ikiwa ni pamoja na kutenga fedha za kutosha, kutumia usafiri bora, kuhifadhi nyaraka muhimu, kuandaa chakula na kinywaji, pamoja na kuzingatia muda wa sala.

### Tatu, kuaga waumini na familia

Mtume (rehema na amani zimshukie) alikuwa akiwaaga waumini na familia yake kabla ya kuanza safari kwa kusema: "Nawaacheni katika ulinzi wa Allah, dini yenu, uaminifu wenu, na matendo yenu ya mwisho." [Tirmidhi].

### Nne, kuteua kiongozi wa msafara

Ikiwa wasafiri ni watatu au zaidi, wanashauriwa kumteua mmoja wao kuwa kiongozi. Mtume wa Allah amesema: "Watu watatu wakiwa safarini wamfanye mmoja wao kiongozi." [Abu Daudi].

### Tano, wanawake kusafiri na maharimu

Kutoka kwa Abu Huraira (radhi za Allah ziwe juu yake) ameeleza kuwa, Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Si halali kwa mwanamke anayemwamini Allah na Siku ya Mwisho kusafiri mwendo wa siku moja bila maharimu." [Bukhari na Muslim].

### Sita, kusafiri siku ya Alhamisi

Imepokewa kuwa Mtume wa Allah (rehema na amani zimshukie) alikuwa akipenda kusafiri asubuhi ya siku ya Alhamisi.

Wanazuoni wanaeleza kuwa kuchagua siku hii kulihusiana na kuanza safari kwa wakati mzuri wa mwanzo wa siku, hali inayomwezesha msafiri kupanga vyema ratiba yake na kufika mapema anakoelekea. Aidha, kufanya hivyo ni sehemu ya kuiga mwenendo wa Mtume, jambo ambalo lina thawabu kwa Muislamu.

### Saba, kukithirisha dua na nyiradi

Imesisitizwa kwa msafiri kukithirisha dua na nyiradi zilizopokelewa kutoka kwa Mtume wa Allah. Miongoni mwa dua hizo ni: "Alhamdulillah, Subhanalladhi sakhkhara lanaa haadha wama kunnaa lahuu muqrinin, wa innaa ilaa rabbinaa lamunqalibuun." [Qur'an, 43:13–14].

Maana yake: "Ametakasika aliyemfanya huyu (mnyama) atutumikie, na tusingeliweza kufanya haya wenyewe. Na hakika sisi tutarudi kwa Mola wetu Mlezi." Ewe Allah, tunakuomba katika safari yetu hii baraka na uchamungu.

Pia inahimizwa kusema "Allahu Akbar" unapopanda mlima, "Subhanallah" unaposhuka, na "Audhu bikalimatillahi ttaammaat min sharri maakhalaq" unapoingia katika mji au kijiji.

### Nane, kudumu na udhu

Mtume wa Allah amesisitiza waumini kudumu na udhu wakati wote, hususan wanapokuwa safarini, kwani udhu hulinda usafi wa mwili na roho.

### Tisa, tabia njema safari

Msafiri anapaswa kuwa na tabia njema na kuheshimu haki za wasafiri wengine, ikiwa ni pamoja na kuwa mkarimu, mpole, kuepuka kuangalia haramu, kuwasaidia wengine, na kuwa mnyenyekevu.

Aidha, ikiwa wasafiri wapo katika chombo kimoja au wamekaa chumba kimoja ndani ya usafiri, ni vyema kuomba ruhusa kabla ya kufungua dirisha au mlango. Kadhalika, ni lazima kuzingatia adabu za kijamii kwa kuepuka kuharibu faraja ya wengine, kama vile kuvuta sigara, kuzungumza kwa sauti kubwa kuhusu mambo binafsi, au kutupa taka ovyo.

### Kumi, kurejea nyumbani haraka baada ya safari

Ni sunna kwa msafiri kurejea nyumbani mara tu anapomaliza safari yake, na si kukaa zaidi ya muda unaohitajika. Mtume amesema: "Safari ni sehemu ya adhabu; inazuia chakula chako, kinywaji chako na usingizi wako."


Hivyo, Muislamu akimaliza haja yake anapaswa kuharakisha kurejea kwa familia yake. Vilevile, ni sunna kukumbatiana mnapokutana au mnaporejea kutoka safarini. Anas (Allah amridhie) amesema: "Masahaba wa Mtume wa Allah walikuwa wakikumbatiana pindi wanapokutana au wanaporudi safari."

ذو القعدة

MAKALA MAALUM

SEHEMU YA 1

Na Said Rajab
0783 650 803




# Hajra, alama ya uongozi na ujenzi wa jamii

**Bi. Hajra, mke wa Nabii Ibrahim na mama wa Nabii Ismail (amani ya Allah iwe juu yao) ni mwanamke mwema aliyechangia kuunda ustaarabu mkubwa wa binadamu, licha ya kwamba hatajwi sana katika historia za kidini.**

Hakuna taarifa nyingi za akiolojia zinazopatikana kuhusu maisha, nasaba au familia yake. Maelezo yaliyopo katika Agano la Kale (Biblia) yanamdhihirisha Hajra kama mtu asiye na shukrani kwa Sara, mke wa kwanza wa Nabii Ibrahim (amani ya Allah imshukie).

Agano la Kale pia linampa hadhi ya suria, huku mwanawe Ismail akioneshwa kama mtoto mwenye wivu kwa mtoto wa Sara, Nabii Is–haka. Wanazuoni wa Kiislamu nao hawakuzingatia kwa kina mchango wake halisi kwa ubinadamu, hususan katika ujenzi wa jamii ya kimataifa ya wanaomuamini Mungu Mmoja, akiwa peke yake jangwani.

Ingawa Qur'an Tukufu imeeleza vizuri kujitoa kwake na nafasi yake katika ibada ya Hijja, wanazuoni wengi hawakulipa uzito wa kutosha suala la chimbuko la maisha ya Hajra na mafunzo yanayopaswa kupatikana kupitia kwake.

Hajra alikuwa binti mdogo mwenye mtoto mchanga anayenyonya. Ni vigumu kwa mwanamke yeyote kufikiria kwamba, Nabii Ibrahim, ambaye alimpata mtoto huyo kimiujiza akiwa katika umri wa uzee, angeweza kumuacha mkewe na mwanawe katika eneo kame lisilo na rasilimali za kutosha kwa maisha yao.

Bila kujali maelezo yanayotolewa na wengine, kitendo hicho kingeonekana kwa wengi kuwa ni kutowajibika. Hata hivyo, Nabii Ibrahim anayejulikana kama rafiki wa Mwenyezi Mungu na mfano wa kuigwa kwa wanadamu alifanya hivyo.

Kwanini? Hebu turejee dua ambayo Nabii Ibrahim aliomba alipomwacha mkewe na mtoto wake mchanga katika jangwa la Arabia: "Mola wetu! Hakika mimi nimewaweka baadhi ya dhuria (familia) wangu katika bonde lisilokuwa na mmea wowote, kwenye Nyumba yako Tukufu (Al–Ka'ba), ewe Mola wetu, ili wasimamishe swala. Basi zijaalie nyoyo za watu zielekee kwao na waruzuku mazao ili wapate kushukuru." [Qur'an, 14:37].

Dua hiyo haikuwa ombi tu kwa Mwenyezi Mungu, bali pia ilikuwa mpango aliokabidhiwa Hajra, ambaye ndiye alikuwa mtu mzima pekee katika bonde hilo.

Mpango huo ulikuwa na malengo manne. Kwanza, watu wanapaswa kuunda jamii yenye imani ya Mungu Mmoja na kumuabudu Yeye pekee. Pili, watu wanapaswa kuwaita wengine kila wakati kwenye dhana ya upekee wa Muumba na kuwashawishi kuhusu ukweli na uthabiti wake.

Tatu, watu wanapaswa kufanya kazi kwa bidii ili kupata riziki ya halali hata katika mazingira yenye ukame. Nne, watu wanapaswa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutumia rasilimali zake kwa usahihi, usawa na bila kufuja.

Kazi kubwa ya Hajra (amani ya Allah imshukie) ilikuwa kuwaongoza wale waliokaa karibu na kisima cha Zamzam katika njia ya Mwenyezi Mungu, sambamba na kumlea mwanawe (Ismail) ili aje kuwa kiongozi.

Mwenyezi Mungu alimuongoza Nabii Ibrahim kumuacha Hajra na mwanawe katika nchi kame, na kupitia kujitolea, uvumilivu, ustahimilivu, mahangaiko na imani yake kwa Mwenyezi Mungu, Hajra alithibitisha kwamba wanawake wana uwezo wa kujenga jamii bora.

*Itaendelea wiki ijayo, Insha Allah*

# TUJIFUNZE

## AI (ARTIFICIAL INTELLIGENCE)

Na Junaynat Ally Dama

SEHEMU YA 1

# Jinsi akili bandia (AI) inavyo badilisha dunia



Katika kipindi cha sasa, ni vigumu kuzungumzia mustakabali wa dunia bila kutaja akili bandia (Artificial Intelligence – AI). Kuanzia majukwaa ya mawasiliano hadi sekta za biashara, elimu na afya, AI imeanza kuingia kwa kasi na kuacha alama inayoonekana. Wengine wanaiona kama injini ya mapinduzi mapya ya kiuchumi, huku wengine wakiiangalia kwa hofu kama chanzo cha kupotea kwa ajira na kudhoofika kwa nafasi ya binadamu.

Swali kuu linalojitokeza si kama AI itabadilisha dunia—hilo tayari linafanyika—bali ni jinsi itakavyofanya hivyo, na nani atanufaika au kuathirika zaidi.

Kwa mujibu wa uchambuzi mbalimbali wa kitaalamu, AI ina uwezo mkubwa wa kuongeza tija katika uzalishaji, kuboresha huduma za afya, na kupanua upatikanaji wa elimu. Haya si madai ya kubuni; ni matarajio yanayotokana na maendeleo ya sasa ya teknolojia. Katika hospitali, kwa mfano, mifumo ya AI tayari inasaidia kugundua magonjwa kwa usahihi mkubwa kuliko mbinu za jadi katika baadhi ya maeneo. Katika elimu, majukwaa ya kujifunza mtandaoni yanayotumia AI yanaweza kubinafsisha mchakato wa kujifunza kulingana na uwezo wa mwanafunzi mmoja mmoja.

Hata hivyo, mtazamo huu wa matumaini haukubaliki kwa wote. Kundi jingine—hasa wale wanaofanya kazi zinazojirudia—linaona AI kama nguvu inayovuruga utulivu wa soko la ajira. Kwao, teknolojia hii si msaada bali ni mbadala. Hoja yao ina msingi: mashine na mifumo ya kiotomatiki zinaweza kufanya kazi nyingi kwa haraka zaidi, kwa gharama ndogo, na bila kuchoka. Katika mazingira kama haya, nafasi ya mfanyakazi wa kawaida inakuwa katika hatari.

Lakini hoja inayozidi kushika uzito katika tafiti nyingi ni kwamba AI haitachukua tu ajira; pia itaunda ajira mpya. Hii si mara ya kwanza katika historia ya binadamu. Mapinduzi ya viwanda yalipokuja, mashine zilichukua kazi nyingi za mikono, lakini pia ziliunda sekta mpya kabisa za ajira. AI inaonekana kufuata mkondo huo huo, ingawa kwa kasi kubwa zaidi.

Takwimu zinaonyesha ukubwa wa mabadiliko haya. Taasisi ya McKinsey Global Institute inakadiria kuwa AI inaweza kuongeza thamani ya uchumi wa dunia kwa takriban dola trilioni 13 ifikapo mwaka 2030. Hii ni sawa na ongezeko la karibu asilimia 16 ya pato la dunia. Kwa lugha rahisi, AI inaweza kuwa kichocheo kikubwa cha ukuaji wa uchumi kuliko teknolojia nyingi zilizowahi kutokea.

Lakini ukuaji huu hautasambazwa sawasawa. Makampuni yatakayoweza kuikumbatia AI mapema yatapata faida kubwa zaidi, huku yale yatakayochelewa yakibaki nyuma. Inakadiriwa kuwa ifikapo mwaka 2030, takriban asilimia 70 ya makampuni duniani yatakuwa tayari yametumia angalau aina moja ya teknolojia ya AI. Hata hivyo, chini ya nusu yao ndiyo yatakayokuwa yameitumia kikamilifu katika mifumo yao yote ya uzalishaji.

Hii inaashiria jambo muhimu: AI si tu teknolojia, bali ni mchakato wa mabadiliko ya kimfumo. Si swali la kuwa na zana, bali ni swali la jinsi ya kuzitumia kwa ufanisi.

Kwa upande wa jamii kwa ujumla, athari za AI zitakuwa pana zaidi ya uchumi. Wachambuzi wanabainisha kuwa AI itaathiri mifumo ya sheria, siasa, na hata maadili ya kijamii. Kadri maamuzi yanavyozidi kufanywa na mifumo ya kidijitali, maswali ya uwajibikaji na haki yatazidi kuwa makubwa. Ni nani anawajibika pale AI inapokosea? Je, tunaweza kuamini mifumo ambayo hatuelewi kikamilifu inavyofanya kazi?

Pamoja na changamoto hizi, kuna makubaliano yanayoibuka polepole kwamba AI, kwa ujumla, inaelekea kuwa nguvu chanya kuliko hasi—lakini kwa masharti. Faida zake zitategemea uwezo wa jamii kujiandaa, kujifunza, na kujiadaptisha kwa kasi inayohitajika.

Kwa kifupi, dunia inaingia katika zama mpya ambapo mstari kati ya uwezo wa binadamu na mashine unaanza kufifia. Wale watakaoweza kuelewa mabadiliko haya mapema na kuyatumia kwa busara watakuwa mbele ya mkondo. Wale watakaoyapinga au kuyapuuza, hatari yao si tu kupitwa, bali kutoweka kabisa katika ushindani wa soko la ajira.

Katika sehemu inayofuata, tutachambua kwa kina jinsi AI inavyobadilisha ajira moja

ذو القعدة

MUSSA IMANI SHEHA ZANZIBAR
0773 181 494

SEHEMU YA 7



# VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

# SIMULIZI YA MTUME MUSA (AMANI YA ALLAH IMSHUKIE)

**Makala yetu katika toleo lililopita ilitufikisha pale Mtume Musa (amani ya Allah imshukie) alipoitwa katika bonde takatifu na kupewa utume rasmi.**

**Musa alipokea wahyi kwa njia ya sauti uliompa misingi ya kitauhidi, kama vile kujua uwepo wa Mmiliki wa viumbe (Allah) na Upweke Wake na imani juu ya Siku ya Mwisho.**

**Alitakiwa kujua kwamba, fimbo na mkono wake sasa vitakuwa ni sehemu ya miujiza atakayoionesha kwa wapinzani wa mafunzo yake.**

**"Na tupa (chini) fimbo yako, basi alipoiona inacheza-cheza aligeuka kwenda zake wala hatazami nyuma (akaambiwa), 'Ewe Musa njoo mbele na usiogope, kwa hakika wewe ni miongoni mwa waliosalimika.'" [Qur'an, 28:31].**

**Baada ya kupokea muujiza huu na ule wa mkono, Nabii Musa (amani ya Allah imshukie) aliambiwa: "...basi hizi zitakuwa dalili mbili zitokazo kwa Mola wako kwenda kwa Fi-aun na wakuu wenziwe, hakika hao ni watu maasi." [Q ur'an, 28:32].**

## Musa kutumwa kwa Fir-aun, apatiwa msaidizi

Allah Ta'alaa akamwambia Musa: "Nenda kwa Fir-aun hakika yeye ameasi." Musa alifikiri sana jinsi ya kumkabili na kumfikishia ujumbe wa Allah, mtu aliyejiita mungu, jabari mwenye kiburi na mtesaji, huku akikumbuka kosa alilowafanyia la kumuua mtu akakimbia!

Katika hali hiyo ya wasiwasi na kujihofia nafsi yake, alisema: "Ewe Mola wangu, hakika mimi nilimuua mtu katika wao, kwa hiyo naogopa wataniua." [Qur'an, 28:33]. Aliongeza udhuru mwengine kwamba, ulimi wake una fundo, hawezi kutamka vyema maneno.

Lakini Mola wake alikuwa anayajua yote hayo, akamwambia nenda tu hayo yatakuwa mepesi kwako.

Nabii Musa akasema: "Ewe Mola wangu, nikunjulie kifua changu, (niweze kuhimili balaa za watu hawa) na uniwepwesishie jambo langu (hii) na unifungulie fundo lililo katika ulimi wangu, wapate kufahamu maneno yangu, na unifanyiye waziri (msaidizi) katika jamaa zangu, ndugu yangu Haruna, nitie nguvu kwaye, na umshirikishe katika kazi yangu (hii). [Qur'an, 20:25-32].

## Musa akumbushwa alikotoka, ahamasika

Maombi ya Mtume Musa yalikubaliwa na pia akahakikishiwa kwamba, ataendelea kuwa katika ulinzi wa Mwenyezi Mungu wakati ujao kama alivyolindwa utotoni mwake. Allah alimkumbusha mazito aliyoyapitia mpaka hapo alipofika.

"(Allah) Akasema: Hakika umekubaliwa maombi yako ewe Musa, na bila shaka tulikufanyia ihsani (fadhila kubwa) mara nyingine (nyingi, kumbuka) tulipomfunulia mama yako yaliyofunuliwa (mara tu baada ya kukuzaa) yakwamba, mtie (mwanao) sandukuni, kisha litupe mtoni, na mto utamtupa fukweni ili amchukuwe adui yangu na adui yake (Fir-aun), na nimekutilia mapenzi yanayotoka kwangu (ili upendwe na watu katika kasri la adui yako), na ili ulelewe machoni mwangu.

(Kumbuka) dada yako alipokwenda (kwa watu wa Fir-aun) akasema, 'Je nikujuilisheni watu wa (kuweza) kumlea?' Na tukakurudisha kwa mama yako ili macho yake yaburudike.

"Na (kumbuka) ulimuua mtu na tukakuokoa katika huzuni, na tukakujaribu kwa majaribu mengi, na ukakaa miaka mingi kwa watu wa Madyan, kisha umekuja hapa kama ilivyokadiriwa ewe Musa. Na nimekuchagua kwa ajili yangu (uwe Mtume)" [Qur'an, 20:36-41].

Kumbukumbu hizi bila shaka ziliujenga vyema moyo wa Mtume Musa kiimani, na kumzidishia yakini kwamba, anayo nguzo imara ya kuitegemea inayosimamia maisha yake, na kamwe maadui zake hawatomfikia.

Kumbukumbu ilimpa hamasa na ushujaa wa kuibeba risala (ujumbe) mzito na kuufikisha kwa watu waliomkufuru Allah na kujipa mamlaka yake, kuwadhulumu watu, na kuharibu miji na vizazi.

Allah aliwaambia: "Msiogope, mimi niko pamoja nanyi, nasikia na naona" [Qur'an, 20:45].

## Mafunzo kwa wanada'wa

Walinganiaji wana ya kujifunza kutoka katika kipengele hiki katika simulizi ya Mtume Musa, ikiwemo mosi, umuhimu wa ufasaha kwa mlinganiaji.

Moja ya maana za ufasaha ni mzungumzaji kutumia lugha iliyozoweleka na kutumiwa na hadhira anayosema nayo, na kutumia misamiati muwafaka kulingana na mahala na watu unaozungumza nao. Da'wa si kupaza sauti kwa jazba na vishindo, huku ukitumia misamiati migumu mpaka watu wanaondoka wakiulizana, "Wewe umemfahamu alichoongea? Mbona mimi sikumuelewa!" Huku dai (mlinganiaji) akijiliwaza kwamba ametekeleza wajibu wake wa kufikisha ujumbe, kumbe wala haukufika.

Kwa kuujua umuhimu huo, Mtume Musa alimuomba Mola wake kwa kusema: "Na ndugu yangu Haruna yeye ni fasaha zaidi kushinda mimi kwa kuzungumza, basi mtume pamoja nami awe msaidizi kunisadikisha, hakika mimi naogopa kwamba watanikadhibisha." [Qur'an, 28:34].

MAKALA
YA AFYA

Na Junaynat Ally Dama



# Bangi inaweza kukukumbusha tukio lisilowahi kutokea?

Utafiti mpya unaonyesha jambo zito: bangi haififishi kumbukumbu tu, bali inaweza kuongeza uwezekano wa mtu kukumbuka mambo ambayo hayakutokea. Kwa mujibu wa makala ya kisayansi iliyoandikwa na Steve Midway na kuchapishwa katika tovuti ya National Geographic, watafiti wamegundua kuwa THC—kiambato kikuu kinachobadilisha fahamu katika bangi—kinaweza kuathiri si tu uwezo wa kukumbuka, bali pia usahihi wa kumbukumbu yenyewe.

Ili kuelewa hili, ni muhimu kwanza kufahamu jinsi kumbukumbu zinavyofanya kazi. Wanasayansi wanaeleza kuwa kumbukumbu hupitia hatua tatu: ubongo unapopokea taarifa (encoding), unapozihifadhi (consolidation), na unapozirejesha (retrieval). Katika maelezo yaliyotolewa na watafiti wa saikolojia ya dawa katika Chuo Kikuu cha Maastricht, yaliyonukuliwa na National Geographic, dawa kama THC huathiri hatua hizi zote—lakini kwa namna tofauti na zisizo rahisi kutabirika.

Tatizo kubwa linaanza katika hatua ya kwanza, yaani wakati ubongo unapochukua taarifa. THC huingiliana na mfumo wa endocannabinoid, hasa vipokezi vinavyoitwa CB1 ambavyo vipo kwa wingi katika sehemu ya ubongo iitwayo hippocampus, inayohusika moja kwa moja na kumbukumbu. Kwa mujibu wa Profesa Carrie Cuttler wa Chuo Kikuu cha Washington State, kama alivyonukuliwa katika makala hiyo, THC "huingilia mfumo huu kwa nguvu," na kusababisha ubongo kushindwa kuhifadhi kumbukumbu kwa usahihi ule ule wa kawaida.

Matokeo yake ni kwamba kumbukumbu zinazohifadhiwa huwa na mapengo. Lakini ubongo hauachi mapengo hayo wazi. Badala yake, hujaribu kuyajaza. Hapa ndipo kinachoitwa false memory—kumbukumbu ya uongo—hutokea. Makala hiyo ya National Geographic inaeleza kuwa kumbukumbu si kurejesha tukio kama lilivyokuwa, bali ni kulijenga upya. Na pale ambapo taarifa hazikuhifadhiwa kikamilifu, ubongo hutumia uzoefu wa kawaida au matarajio kujaza sehemu zilizokosekana.

Hali hii inaweza kusababisha mtu kuwa na uhakika mkubwa juu ya tukio ambalo halikuwahi kutokea. Mfano uliotolewa katika makala hiyo unaonyesha kuwa mtu anaweza "kukumbuka" alikula chakula fulani kwa sababu ndicho anachokula mara nyingi, hata kama siku hiyo hakukula.




Zaidi ya hapo, tafiti zinaonyesha kuwa THC hubadilisha aina ya kumbukumbu tunazotegemea. Wanasayansi hutofautisha kati ya recollection—kukumbuka kwa undani—na familiarity—hisia ya kwamba jambo linafahamika. Kwa mujibu wa utafiti huo ulioripotiwa na National Geographic, THC hupunguza uwezo wa kukumbuka maelezo maalum, lakini huacha hisia ya "najua hili" ikiwa intact. Hapo ndipo hatari ipo: mtu ana uhakika, lakini si sahihi.

Athari nyingine ni kwenye kile kinachoitwa source memory—uwezo wa kukumbuka chanzo cha taarifa. Makala hiyo inaeleza kuwa mtu anaweza kukumbuka jambo fulani, lakini ashindwe kutofautisha kama alilisoma, alilisikia, au aliliona mtandaoni. Katika mazingira ya taarifa nyingi, hili linaweza kusababisha mtu kusambaza taarifa zisizo sahihi bila kujua.

Ushahidi wa majaribio unaonyesha ukubwa wa tatizo hili. Katika utafiti uliowahusisha watumiaji wa bangi, uliotajwa katika makala hiyo, karibu asilimia 70 ya washiriki walionyesha matatizo ya kumbukumbu chini ya athari za THC. Zaidi ya hapo, walikuwa na uwezekano mkubwa zaidi—karibu mara mbili—wa "kukumbuka" mambo ambayo hayakuwahi kutokea.

Kwa mujibu wa watafiti hao, hali hii inaelezwa na mabadiliko katika ubongo, hasa katika hippocampus. Tafiti zilizochapishwa awali katika jarida la Nature, kama zilivyonukuliwa na National Geographic, zinaonyesha kuwa THC inaweza kuathiri michakato ya nishati ndani ya seli za neva, jambo linalohitajika ili kumbukumbu ziwe thabiti. Bila uthabiti huo, kumbukumbu hubaki dhaifu na rahisi kupotoshwa.

ذو القعدة

# MATUKIO YENYE MAZINGATIO

NA ZAHARANI BARAKA

# Tujifunze ibada ya Hijja kwa Mtume wetu

**Kutoka kwa Saalim bin Abdullah (radhi za Allah ziwe juu yake) amesimulia kuwa alimsikia mtu mmoja kutoka Sham akimuuliza Abdullah bin Umar kuhusu kufanya Umra pamoja na Hajj (tamattu'u). Ibn Umar alijibu kwamba jambo hilo linafaa kisheria.**

**Yule mtu wa Sham akasema: "Lakini baba yako (Umar) alikataza jambo hilo." Ibn Umar akamuuliza: "Unaonaje ikiwa baba yangu alikataza, lakini Mtume wa Allah (rehema na amani zimshukie) alilifanya. Je, tufuate amri ya baba yangu au amri ya Mtume?"**

**Yule mtu akasema: "Tufuate amri ya Mtume (rehema na amani zimshukie)." Ibn Umar akamwambia: "Hakika Mtume alifanya (hivyo)." *[Tirmidhi]*.**

## Mafundisho ya tukio

Kufuata sunna (mwendo) za Mtume (rehema na amani zimshukie) ni jambo linalopewa kipaumbele cha kwanza kuliko maoni ya mtu yeyote au mtazamo wake.

Kuna ibada ambazo mfumo wake ni sehemu ya ibada yenyewe, kwa maana huwezi wala huruhusiwi kuzifanya kwa namna nyingine isipokuwa kwa kumuiga Mtume (rehema na amani zimshukie).

Katika zama hizi, watu wamebadilisha mambo mengi katika sifa au mfumo wa utekelezaji wa ibada mbalimbali na kuzitoa katika uhalisia wake. Si jambo la kushangaza kukuta watu wanafanya ibada ambayo asili yake ni ibada kisharia, lakini namna inavyofanyika inakwenda kinyume na utaratibu wa kisharia.

Tukio hili linaonesha msimamo imara wa Abdullah bin Umar (Allah amridhie yeye na baba yake). Msimamo huu unaakisi hali waliyokuwa nayo Masahaba ya kuipenda haki badala ya kufuata mitazamo ya watu.

Ibn Umar hakujali alipoambiwa kuwa baba yake (Umar) alikataza Hijja ya tamattu'u. Aliamini kwa kile alichojifunza kwa Mtume (rehema na amani zimshukie), na huenda baba yake hakuona au hakujua kuwa Mtume ameelekeza hivyo.

Msingi wa msimamo huu ni kumuiga na kumfuata Mtume katika hatua zote za utekelezaji wa ibada. Haitoshi kuangalia msingi wa ibada tu, bali inatakiwa kujifunza namna inavyotekelezwa ili ibada ikubalike.

## Aina tatu za Hijja

Hijja ni ibada adhimu yenye utaratibu maalumu katika utekelezaji wake, kama zilivyo ibada nyingine. Kuna aina tatu za Hijja ambazo kila hujaji ana uhuru wa kuchagua mojawapo kulingana na nia na uwezo wake wa kukidhi masharti ya kila aina. Aina hizo ni Ifraad, Qiraan na Tamattu'u.

Hijja ya Ifraad ni kutia nia ya Hijja pekee bila Umra. Katika aina hii, hujaji hufanya tawafu ya kuwasili mara saba kisha husali rakaa mbili nyuma ya Maqam Ibrahim.

Aina ya pili ni Qiraan, ambapo hujaji huchanganya Hijja pamoja na Umra kwa kufanya baadhi ya matendo katika ibada zote mbili.

Aina ya tatu ni Tamattu'u, ambapo ibada ya Umra hufanywa kivyake na ibada ya Hijja hufanywa kivyake ndani ya msimu mmoja wa Hijja. Katika aina hizi tatu, Tamattu'u ndiyo aina bora zaidi na yenye nafuu kubwa kwa wale wanaotoka mbali.

## Kubusu jiwe jeusi

Ni sunna kwa hujaji kulibusu jiwe jeusi (Hajar Al–Aswad) kama alivyofanya Umar bin Khattwab, bila ya kulitukuza au kulitegemea kuwa linaweza kuleta manufaa. Mtume (rehema na amani zimshukie) alilibusu jiwe hilo, hivyo Umar akafuata sunna hiyo.

## Kufuata sunna

Inafahamika kuwa katika zama hizi khilafu zimekuwa nyingi mno, hata katika mambo ambayo Mtume (rehema na amani zimshukie) alikuwa akiyafanya.

Watu wanatanguliza maoni, rai na mitazamo ya akili zao huku wakijua fika kuwa utaratibu wa jambo fulani haukuwepo kabisa katika karne za wema waliopita. Njia bora ya kuwaunganisha watu ni kufuata sunna na kuchukia khilafu.

Kutoka kwa Abdurrahman bin Yazid (Allah amridhie) amesema: "Uthman (radhi za Allah ziwe juu yake) alisali Mina rakaa nne."

Pia Abdullahi bin Mas'ud (Allah amridhie) amesema kuwa katika miaka tofauti alisali pamoja na Mtume (rehema na amani zimshukie) rakaa mbili, alisali na Abubakr rakaa mbili, na akasali na Umar rakaa mbili; na mwanzoni mwa utawala wa Uthman alikuwa akisali rakaa mbili, kisha akabadilisha na kusali rakaa nne.

Ibn Mas'ud alisema: "Mmegawanyika katika njia tofauti, na ningependa ningepata katika rakaa nne au rakaa mbili zenye kukubaliwa." Imepokewa pia kuwa, Ibn Mas'ud alisali rakaa nne, mtu mmoja akamuuliza: "Mbona umemkosoa Uthman, halafu wewe unaswali rakaa nne?" Ibn Mas'ud akajibu: "Tofauti (khilafu) ni shari."

Kama inavyoonekana katika tukio hili, tunaweza kufuata sunna na kuondoa dhana ya tofauti ambazo zinaweza kuwasambaratisha watu. Abdullahi bin Mas'ud (Allah amridhie) aliamua kutimiza sala rakaa nne, kama alivyosali Uthman ili kuondoa tofauti.

Ingawa ilikuwa bora kupunguza sala, Uthman aliona kuwa khilafu ni mbaya zaidi kuliko fadhila alizozikosa. Hivyo basi, ili kuepuka mitazamo tofauti ni muhimu kushikamana na sunna (mwenendo wa Mtume) katika ibada zote.

JUNAYNAT ALLY DAMA



# Mtoto ni rehema inayofundisha moyo kupenda

Kuna siku nyumba huwa kimya sana mpaka sauti ya mtoto mmoja mdogo inapobadilisha kila kitu. Kicheko chake kinapenya kwenye uchovu wa maisha kama mwanga wa alfajiri unaopenya dirishani baada ya usiku mrefu. Wakati mwingine hatutambui mapema kuwa watoto hawaji tu kutuletea jukumu la kuwalea, bali pia hutujenga sisi wenyewe.

Mtoto huja duniani akiwa mdogo kwa umbo, lakini mkubwa kwa mafunzo anayobeba ndani yake.

Ni ajabu jinsi moyo wa mtoto unavyokuwa mpana. Mzazi anaweza kukasirika, kupaza sauti, au hata kumwadhibu kwa jambo ambalo halikuwa kosa lake kabisa. Lakini baada ya muda mfupi, mtoto anarudi tena akiwa na tabasamu, akitaka kukukumbatia kana kwamba hakuna kilichotokea. Watoto hawakai na chuki muda mrefu. Hawajui kuweka visasi ndani ya vifua vyao vidogo.

Ndiyo maana wakati mwingine mzazi anatakiwa kujifunza kusema "ahsante" kwa mtoto wake. Ahsante kwa kusamehe haraka. Ahsante kwa kuendelea kupenda hata pale wazazi wanaposhindwa kuwa wakamilifu.

Katika dunia ambayo watu wazima wengi huweka majeraha mioyoni kwa miaka mingi, watoto hutufundisha namna ya kuachilia na kuanza upya.

Na kuna jambo jingine la ajabu zaidi. Watoto huwa upande wetu hata pale dunia nzima inapokuwa mbali nasi. Mkono mdogo wa mtoto unaposhika kidole cha mzazi, huwa kama ujumbe wa kimya unaosema: "Mimi niko hapa." Kwa mtoto mdogo, mzazi wake ndiye dunia nzima. Ndiye usalama wake, furaha yake na sehemu yake ya kupumzika.

Pengine ndiyo maana uwepo wa mtoto huifanya nyumba iwe tofauti. Si kwa sababu ya kelele zao tu, bali kwa sababu hujaza nafasi za moyo ambazo hatukujua zilikuwa tupu.

Baada ya siku ndefu yenye uchovu, msongo wa mawazo na mapambano ya maisha, tabasamu la mtoto linaweza kuondoa uzito wote wa dunia ndani ya dakika chache. Kicheko chao huwa safi, hakina unafiki, hakina kujifanya. Ni kicheko kinachotoka moyoni moja kwa moja. Mtoto mmoja anaweza kucheka kwa jambo dogo kabisa, na ghafla mzazi naye anajikuta anacheka. Kama vile watoto wameumbwa na uwezo wa kuwasha tena nuru ndani ya mioyo iliyochoka.

## Lakini watoto hawatuletei furaha pekee. Hutubadilisha pia.

Watu wengi wanapopata watoto, huanza kuona maisha tofauti. Wanaanza kuwa wavumilivu zaidi, wenye huruma zaidi, na wenye kuwaza zaidi kuhusu kesho. Mtoto anakufundisha kuwajibika bila kukufundisha darasani. Anakufundisha kujitoa bila kukusomea kitabu.

Kupitia watoto, watu wengi hugundua mapungufu yao na kujifunza kuwa bora zaidi. Wengine hujifunza kudhibiti hasira. Wengine hujifunza upole. Wengine huanza hata kumkaribia zaidi Mwenyezi Mungu kwa sababu wanaona ukubwa wa amanah waliyopewa.

Na pengine jambo la kugusa zaidi ni namna watoto wanavyotufanya tujisikie wa muhimu.

Katika miaka yao ya mwanzo, watoto hawahitaji sana vitu vya gharama. Wanahitaji uwepo wetu. Wanataka kukaa karibu nasi, kusikiliza sauti yetu, kushikwa mkono wetu, au kulala kifuani mwetu. Kwao, uwepo wa mzazi ni usalama ambao hakuna fedha inayoweza kununua.

Mtoto anapokukimbilia baada ya kuogopa, anapokuita kwa furaha unapofika nyumbani, au anapolala huku ameshika mkono wako, moyo wa mzazi hupata hisia ambazo ni vigumu kueleza kwa maneno.

## Ndiyo maana watoto wanastahili shukrani zetu.

Si kila shukrani lazima iwe zawadi kubwa. Wakati mwingine ni maneno madogo tu kabla hawajalala: "Asante kwa kunifanya kuwa baba," au "Asante kwa kunifanya kuwa mama." Maneno hayo yanaweza kujenga ndani yao hisia ya kuthaminiwa na kuimarisha mapenzi kati ya mzazi na mtoto.

UKHTI FATIMA SS

# Kwa nini watu wenye akili kubwa hujikuta wapweke zaidi?



Kwa kawaida, jamii huamini kuwa mtu mwenye akili kubwa ana nafasi nzuri zaidi ya kufanikiwa maishani. Anaweza kufanya vizuri shuleni, kazini au katika kutatua changamoto mbalimbali. Lakini tafiti za saikolojia zinaonyesha kuwa nyuma ya uwezo huo mkubwa wa kufikiri, mara nyingi kuna changamoto nyingine inayojificha: upweke.

Makala iliyochapishwa na jarida la Psychology Today inaeleza kuwa watu wenye akili kubwa mara nyingi huwa na mahitaji ya kijamii tofauti na watu wengine. Wanaweza kupenda kuwa peke yao zaidi, kuchoshwa haraka na mazungumzo ya kawaida, au kuhisi hawapati watu wanaowaelewa kwa kina.

Jambo hili halimaanishi kuwa watu wenye akili kubwa wanawachukia wengine. Hapana. Mara nyingi tatizo huwa namna akili zao zinavyofanya kazi. Wataalamu wanaeleza kuwa watu hawa hupenda mijadala yenye kina, fikra nzito na mazungumzo yenye maana kubwa kuliko mazungumzo ya kawaida ya kila siku.

Kwa mfano, mtu mwenye akili nyingi anaweza kutumia saa nyingi kufikiria mradi, kuandika, kusoma au kutatua tatizo gumu. Baada ya kutumia nguvu nyingi za akili, anaweza kukataa kwenda kwenye mkusanyiko mkubwa wa watu. Wengine wanaweza kuona ni mtu asiyechangamana, lakini ukweli ni kwamba akili yake tayari imechoka kutokana na shughuli nzito za kufikiri.

Utafiti uliohusisha zaidi ya vijana 15,000 uligundua jambo la kushangaza. Watu wengi walionyesha kuwa furaha yao huongezeka wanapokutana mara kwa mara na marafiki. Lakini kwa watu wenye kiwango kikubwa cha akili, hali ilikuwa tofauti. Kadiri walivyokuwa wakishiriki sana katika mikusanyiko ya kijamii, ndivyo kiwango cha kuridhika kwao maishani kilivyopungua.

Watafiti wanaeleza jambo hili kupitia kile wanachokiita "Savanna Theory." Nadharia hii inaeleza kuwa binadamu waliumbwa kuishi katika jamii ndogo zenye ukaribu mkubwa, kama ilivyokuwa zamani katika mazingira ya asili. Ndiyo maana watu wengi hupata furaha wanapokuwa karibu na wengine.

Hata hivyo, watu wenye akili kubwa wana uwezo mkubwa zaidi wa kuzoea maisha ya kisasa yenye kujitegemea. Wanaweza kujitosheleza kihisia kupitia kazi zao, ubunifu, malengo ya muda mrefu au shughuli za kiakili. Kwao, muda wa kutafakari au kufanya kazi ya kina unaweza kuwa wenye maana zaidi kuliko kutumia muda mwingi kwenye mazungumzo yasiyo na lengo.

Tatizo jingine ni kwamba watu wenye akili kubwa mara nyingi hupata ugumu wa kupata watu wanaolingana nao kiakili. Upweke si kukosa watu karibu yako pekee. Wakati mwingine unaweza kuwa umezungukwa na watu wengi lakini bado ukahisi hakuna anayekuelewa.

Watu wenye akili nyingi huwa na uwezo mkubwa wa kuchambua mambo kwa kina, kuona uhusiano wa mambo mbalimbali na kuhoji masuala kwa namna tofauti. Lakini mazingira mengi ya kijamii hujengwa juu ya mazungumzo mepesi, utani wa kawaida au mada zinazojirudia. Kwa mtu anayependa fikra pana na za kina, hali hiyo inaweza kuonekana ya kuchosha.

Mwishowe, baadhi yao hulazimika kuficha namna yao halisi ya kufikiri ili waweze kuendana na wengine. Anaweza kujizuia kuzungumza mawazo yake kwa kina kwa sababu anaogopa kuonekana "anawaza sana" au tofauti na wengine. Hali hii inaweza kuleta kile kinachoitwa "existential isolation," yaani hisia kwamba hakuna anayeelewa ulimwengu wako wa ndani.

Hata hivyo, wataalamu wanasisitiza kuwa kuwa peke yako si sawa na kuwa mpweke. Kuna tofauti kati ya "solitude" na "loneliness." Mtu anaweza kuchagua kukaa peke yake ili kufikiri, kuandika au kufanya ibada na akahisi amani kabisa. Huo si upweke mbaya. Tatizo linaanza pale mtu anapohisi hana mahusiano ya kweli ya kumwelewa na kumkubali alivyo.

Katika mtazamo wa Kiislamu, Uislamu unahimiza mizani. Muislamu anatakiwa kuwa na muda wa kutafakari, kufanya ibada na kujenga nafsi yake, lakini pia kushirikiana na jamii. Mtume Muhammad (rehema na amani zimshukie) aliwahimiza Waislamu kudumisha undugu, kuwatembelea watu na kusaidiana.